# Nipashe

Jumanne Julai 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581732

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





**Baba** wa kambo mbaroni tuhuma kumnyonga mtoto hadi kufa

UKURASA 3




**Makonda**: Nitajieni wanaokwamisha kesi za ubakaji, ulawiti nipambane nao

UKURASA 4

**CCM** yaahidi kusimamisha wagombea chaguo la wananchi

UKURASA 5



Boniface Mwabukusi

Peter Kibatala

UKURASA 2

# Joto la uchaguzi lapamba moto TLS

UKURASA WA 21

## DESCHAMPS AMTETEA MBAPPE KIWANGO EURO



KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amemtetea nahodha wake na mchezaji nyota, Kylian Mbappe, baada ya kukosolewa kutokana na uchezaji wa mshambuliaji huyo katika michuano ...

**KASORO UJENZI WA SHULE**

## PM achukizwa aagiza mhandisi halmashauri kusimamishwa

UKURASA 4




Wafanyabiashara wa kituo cha daladala cha Simu 2000 Ubungo jijini Dar es Salaam wakigoma kuhamishwa kutoka katika eneo lao la biashara kwa kile kilichodaiwa kupisha ujenzi wa karakana ya mabasi ya Mwendokasi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chalamila azima mgomo w'biashara Simu 2000

UK. 2


**MICHEZO** YANGA SC KUIFUATA KAIZER CHIEFS SAUZI UK.24 **MAONI,** UK.6



Aliyekuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (kushoto) akimkabidhi ofisi Kamishna Mkuu mpya, Yusuph Mwenda. Hafla hiyo ya makabidhiano imefanyika katika Ofisi za TRA Makao Makuu Dar es Salaam jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Joto uchaguzi TLS lapanda

**Na Restuta James**

JOTO la uchaguzi wa rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), limeendelea kupanda, huku baadhi ya mawakili wakipinga kuenguliwa kwa mgombea wa nafasi hiyo, Boniface Mwabukusi.

Tofauti na vyama vingine vya kitaaluma, uchaguzi wa TLS umekuwa na mguso wa pekee kwa jamii ukitikisa ndani ya chama na kwenye mitandao ya kijamii.

Jana, wakili Peter Kibatala, alisema kuenguliwa kwa Mwabukusi kunaufanya uchaguzi uwe na maswali mengi kwa kuwa tuhuma za maadili zilizomwengua, hazina mashiko.

Alisema kuishtaki serikali ni jambo la kawaida wala hakupingani na sheria wala Katiba ya nchi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kibatala alisema kamati iliyomwengua ina uwezo wa kumrejesha kuwania kiti hicho, akikumbusha kuenguliwa kwa aliyekuwa mgombea urais wa TLS, John Seka, mwaka 2016.

"Sio lazima awe mgombea wangu na wala nisingemchagua Mwabukusi kwa sababu zangu... kama unakumbuka kamati iliwahi kumwengua John Seka, nikasimama ukumbini kuiambia kamati kwamba walikosea kumwondoa, wakamrejesha na akashinda urais, maana yake ni kwamba walimwengua mtu ambaye alikuwa chaguo la watu na wasingemrejesha ni kwamba tungepata mtu asiye sahihi," alisema.

Alisema mawakili wanatumia njia za kisheria kudai haki. "Sisi sio marubani au madaktari, tutajua nini cha kufanya maana ndicho tulichokisomea."

Awali, katika andiko lake kwenye mitandao ya kijamii, Kibatala alisema ataendelea kupinga mchakato wa uchaguzi na kususia mikutano akieleza kuwa chama hicho ndio ukuta wa mwisho wa kuulinda umma.

"Nitashiriki kuwashawishi wengine wafanye hivyo, kwa wakati huu nitashirikiana na wakili Mwabukusi katika kusaka haki yake ya kisheria. Kwa hali ilivyo, sioni kuna uchaguzi halali ndani ya TLS," alisema Kibatala.

Mmoja wa wagombea urais, Kapteni Ibrahim Bendera, alisema uamuzi wa Mwabukusi kwenda mahakamani ni sahihi kwa kuwa ni chombo cha kutoa haki.

"Hatuwezi kulazimisha kamati imrejeshe, lakini naamini mahakamani atapata haki stahiki. Mwenyewe keshasema atakata rufaa, tusubiri maamuzi ya mahakama na matokeo ya rufaa," alisema.

Alisema anawania ili aongoze Baraza la Uongozi kuboresha taaluma ya uwakili; kuwasaidia na kuwaelimisha mawakili wenye uzoefu wa chini ya miaka mitano ambao hawaruhusiwi kuingia Mahakama ya Rufani; kupunguza ada ya kila mwaka; kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuwekeza kwenye vitega uchumi katika kila tawi la TLS.

Kwenye mitandao ya kijamii, baadhi ya wanaharakati wameunga mkono uamuzi wa Mwabukusi kushinikiza arejeshwe kuwania nafasi hiyo, wakieleza kuwa ana haki kisheria na kikanuni.

**SARAKASI**

Kwa miaka mingi, uchaguzi wa TLS umekuwa ukivuta hisia za wananchi ndani na nje ya chama hicho, huku sarakasi zikitawala.

Mwaka 2016, Seka alienguliwa na baada ya mawakili 'kuijia juu' kamati ya uchaguzi, ilimrejesha na akachaguliwa kuongoza chama hicho.

Uchaguzi wa TLS umekuwa wa mchakamchaka kutokana na majukumu yake ambayo ni pamoja na kuishauri serikali na taasisi zake. TLS ilianzishwa kwa sheria mwaka 1954 kama chama cha kitaaluma cha mawakili nchini na kifungu cha 4 cha sheria hiyo (Sheria ya Chama cha Mawakili wa Tanganyika), inabainisha majukumu makuu matatu ya taasisi hiyo.

Jukumu la kwanza, ni kuwaunganisha, kuwatetea na kusaidia ustawi wa mawakili nchini. Pili, ni kuishauri Serikali na vyombo vyake kama Bunge na Mahakama. Jukumu jingine ni kusimamia maslahi na ustawi wa jamii ya Watanzania.

Kutokana na nguvu hiyo, chama hicho kimekuwa kikipitia nyakati tofauti za viongozi kulingana na wakati husika. Kuanzia mwaka 2016, TLS ilikuwa na viongozi waliokuwa mstari wa mbele kuikosoa serikali akiwamo Fatma Karume, ambaye jina lake lilienguliwa mwaka 2019.

Jukumu jingine ni kusimamia maslahi na ustawi wa jamii ya Watanzania. Majukumu hayo yanasababisha jamii ifuatilie kwa ukaribu uchaguzi wake.

Baadhi ya viongozi wa TLS waliokuwa mwiba kwa serikali ni pamoja na Tundu Lissu, aliyekuwa Rais wake mwaka 2017, na katika kipindi chake, kulikuwa na msuguano mkali kati ya TLS na serikali.

Serikali iliituhumu TLS kufanya siasa kwa kukosoa kazi zake, badala ya kujielekeza kwenye malengo ya kuanzishwa kwake, jambo ambalo lilizidisha migongano baina ya pande hizo mbili.

Kutokana na hali hiyo, Machi 2017, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Harrison Mwakyembe, alitishia kukifuta chama hicho.

Hata hivyo, baada ya Lissu, mwanaharakati ambaye alikuwa mkosoaji wa serikali, Fatma Karume, alichaguliwa kuiongoza TLS. Mwaka uliofuata, alisimama kutetea nafasi yake kwa awamu nyingine, lakini jina lake halikurejeshwa.

Wakati wa uongozi wa Fatma, misuguano kati ya TLS na serikali ilishika kiasi cha kuonekana chama hicho kimebeba agenda za kiharakati.

Septemba 20, 2019, Fatma alisimamishwa uwakili na Mahakama Kuu kwa madai ya kuishambulia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na alifikishwa mbele kamati ya maadili ya mawakili kujadiliwa. Kamati hiyo ilimfutia uwakili, hata hivyo, alirejeshewa tena Juni 21, 2021.

Baada ya Karume, alichaguliwa Profesa Edward Hosea, aliyekuja na sera ya sera ya majadiliano ya kujenga, kwa maana ya kukaa pamoja na serikali ambayo ni mdau muhimu ili kufanyakazi kwa ushirikiano, na katika uchaguzi wa kwanza, Hosea aliibuka kidedea kwa kumwangusha aliyeonekana kuwa mpinzani wake mkubwa, Harold Sungusia.

Sungusia ndiye rais wa TLS anayemaliza muda wake wa uongozi akiwa amehudumu vipindi viwili mfululizo.

# Chalamila azima mgomo w'biashara Simu 2000

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amewataka wafanyabiashara wadogo maarufu machinga katika soko la Simu 2000 kusitisha mgomo na kuendelea na majukumu yao huku akiwaahidi kuzungumza nao Julai 13, mwaka huu, kuwapa msimamo wa serikali.

Jana wafanyabiashara hao waligoma na kuziba barabara kuzuia magari kuingia katika kituo cha mabasi wakilalamikia uamuzi wa kukabidhi eneo hilo kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ili kujenga karakana.

Akizungumza na wafanyabiashara hao jana, Chalamila alikiri suala hilo lipo, lakini halijafikishwa ofisini kwake ili atoe uamuzi kwa kuwa alimwagiza Mkuu wa wilaya hiyo, Hassan Bomboko, walijadili kwanza kwenye mikutano ya wilaya kisha wampelekee.

Aliwaomba wampe muda ili azungumze na DART, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Manispaa ya Ubungo na kuja kuzungumza nao ili wawaeleze msimamo wao.

Alisema suala hilo linahitaji umakini katika kulitafutia ufumbuzi kwa kuwa wafanyabiashara hao wamehangaishwa kwa kuhamishwa maeneo.

"Jambo la kwanza siku nyingine mimi kaka yenu nipo, jambo lolote likitokea Ofisi ya RC (Mkuu wa Mkoa) ipo wazi, kabla hamjachukua uamuzi wowote jiridhisheni pia RC analijua hili? Pamoja na kwamba shughuli zimesimama nitakapoondoka hapa endeleeni na shughuli zilizopo," aliagiza.

Awali, Mkuu wa wilaya Bomboko alifika kwa ajili ya kuzungumza na wafanyabiashara hao, lakini walikataa kuzungumza naye na kumtaka aondoke kwa madai kuwa hawana imani naye.

Machinga hao walisema wamelalamikia mara kwa mara kuhusu changamoto zinazowakabili katika eneo hilo na kuwaahidi kwenda kuzifanyia kazi, lakini hakufanya hivyo.

**DC ASHANGAZWA**

Akizungumza na waandishi wa habari, Bomboko alisema anashangazwa na uamuzi waliochukua wafanyabiashara hao kwa kuwa hakuna taarifa zozote kuwa eneo hilo limekabidhiwa kwa DART.

Aidha, alisema walikuja hapo kujiridhisha kama kweli wafanyabiashara hao wamesitisha shughuli zao kutokana na madai hayo na kutaka kufahamu kutoka kwao kuwa taarifa hizo zimetangazwa na kiongozi gani wa serikali.

"Manispaa ya Ubungo ndio iliwajengea wafanyabiashara hao vibanda na ndio wamiliki wa eneo hilo, kwa maana hiyo kama kulikuwa na mabadiliko ya matumizi viongozi wa manispaa ndio walitakiwa kutoa taarifa kwa wafanyabiashara," alisema.

"Lakini hoja ya kwamba soko hili limeuzwa kwa Wachina ni taarifa ambayo na mimi ninaisikia kutoka kwenu, ndio maana nilitaka kujua kutoka kwa wafanyabiashara ni Mchina gani aliyenunua hili soko, lakini pia hizi taarifa zimetangazwa na kiongozi gani wa serikali," alihoji.

Alisema kilichofanyika katika eneo hilo ni vita za kisiasa ili serikali iache kufanya masuala ya msingi na kuacha mambo yaende kiholela, aliwasihi wafanyabiashara waendelee na biashara zao na wenye malalamiko waende ofisini wakazungumze.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Iddi Ramadhani alisema, hawakubaliani na uamuzi wa kuwaondoa wafanyabiashara 2000 na kuweka kituo cha DART chenye magari takribani 230, jambo ambalo si la kiungwana.

"Sisi ni wafanyabiashara tuliotoka barabarani na kuja kukaa sokoni kwa kuheshimu kauli ya Rais Samia, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alituthibitishia kuwa hili ni soko na tukae kwa amani, leo mtu anakuja anakwambia kuwa wamebadilisha matumizi anatakiwa apewe DART, kwamba DART anathamani kuliko sisi tuliowekeza kwa miaka sita," alihoji.

# Baba wa kambo mbaroni tuhuma kumnyonga mtoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia, Stephen Mabula ambaye ni baba wa kambo wa Godluck Mathias (5), kwa tuhuma za kumnyonga hadi kufa mtoto huyo.

Pia, linaendelea na msako wa mtu mmoja anayetuhumiwa kwa mauaji ya wasichana wawili waliochomwa moto eneo la Nzuguni, jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, Theopista Mallya, alisema tukio la baba wa kambo kumuua mtoto huyo limesababishwa na ulevi.

Alisema baada ya kulewa aligombana na mke wake ambaye ndiye mama mzazi wa mtoto aliyeuawa.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa baada ya ugomvi uliotokana na ulevi, mama wa mtoto huyo alikimbilia kwa majirani ndipo baba huyo inasadikiwa alimchukua mtoto na kumnyonga hadi kufa.

Kamanda Mallya alisema tukio hilo limetokea jana katika Kijiji cha Mihema, wilayani Chamwino mkoani Dodoma na Polisi inaendelea na uchunguzi.

Alisema tukio hilo linahuzunisha na kuitaka jamii kuwa makini na watoto kunapotokea ugomvi wa wazazi.

Alisema mwili wa mtoto huyo unatarajiwa kuzikwa katika Kijiji cha Mwitichila, wilayani Bahi, mkoani hapa.

Hata hivyo, alisema ugomvi wa wazazi haupaswi kuwahusisha watoto wadogo na kuwapotezea maisha.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya majirani wa mama mzazi wa mtoto aliyefariki walisema baba huyo ni mganga wa kienyeji na hana shughuli nyingine.

Mmoja wa majirani hao, Anna Yohana, alisema tukio hilo limeleta simanzi kubwa kijijini hapo kwa sababu mtoto aliyefariki hakuwa na kosa lolote na baba huyo hakupaswa kufanya kitendo cha mauaji dhidi ya kijana huyo.

Pia, Kamanda Mallya alisema Jeshi la Polisi halikubaliani na vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa raia, ndio maana limekuwa likifanya msako kila kona ya Jiji la Dodoma ili kuwakamata wahalifu.

# Mabadiliko Sheria Uchaguzi yampa imani Bob Wangwe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKURUGENZI wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Zakayo Wangwe maarufu kama Bob Wangwe, amesema baadhi ya mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Uchaguzi yanatia imani kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu 2025.

Bob Wangwe alitoa kauli hiyo juzi Tarime Mjini akihutubia mkutano wa hadhara wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuondoa baadhi ya urasimu uliokuwa ukifanyika katika uchaguzi.

"Zamani sheria za uchaguzi zilikuwa zinataja sifa moja wapo ya msimamizi wa uchaguzi kuwa ni mkurugenzi wa halmashauri au manispaa, lakini leo kwasababu tulipeleka kesi mahakamani, tukawashinda mahakama kuu hadi mahakama ya Afrika wakapewa miezi 12 kurekebisha sheria ambazo kwa sasa zimesaidia kuondoa hilo tatizo," alisema.

Alisema katika sheria za sasa miongoni mwa sifa zilizotajwa ni pamoja na kuwa mtumishi mwandamizi pamoja na kutokuwa kada wa chama chochote cha siasa.

"Zamani hiyo haikuwapo maana hata kama wataamua kutumia wakurugenzi watatumia wale ambao sio makada, lakini awali alikuwa anaweza kuteuliwa Mwenyekiti wa CCM au aliyeshindwa kwenye kura za maoni anateuliwa kuwa mkurugenzi na kusimamia uchaguzi," alisema Wangwe.

Licha ya kuwa bado wanaendelea na madai ya Tume Huru pamoja na Katiba mpya, alisema kwa sasa wanaona mabadiliko hayo kwa kuanzia ni mazuri katika kupata sauti ya wananchi kwenye vyombo vya maamuzi.

Aliomba kuwapo kwa uchaguzi usiokuwa na vurugu na kutoa fursa kwa wananchi kupitisha watu ambao ndio machaguo yao, huku akiwataka wagombea wote kutokubali vitisho vya aina yoyote vinavyolenga kubatilisha nia na haki zao za kugombea nyadhifa mbalimbali.

Aprili 2, 2024, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliliambia Bunge kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia na kutia saini kwenye miswada hiyo minne iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa 14 ambayo ni Muswada wa Sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya vyama vya Siasa pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba tano, yote ya mwaka 2023.

"Sasa hizi zimekuwa sheria za nchi na zitaanza kuitwa kwa majina yafuatayo: Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Namba moja ya mwaka 2024, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi namba mbili ya mwaka 2024,"

"Nyingine ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa namba tatu ya mwaka 2024, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba nne ya mwaka 2024, kwahiyo waheshimiwa wabunge hizi tayari zimekuwa sheria kamili Mhe. Rais ameishafanya kwa sehemu yake," alisema Spika Dk.Tulia.

Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com



**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5

For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# PM achukizwa aagiza mhandisi halmashauri kusimamishwa kazi

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, ameagiza kusimamishwa kazi mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Emmanuel Sigachuma baada ya kukuta kasoro mbalimbali za ujenzi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Lugalo, iliyopo wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Pia, ameagiza Ofisa Elimu wa Sekondari, Nelson Milanzi apewe onyo kwa kushindwa kusimamia matumizi ya fedha za ujenzi wa shule hiyo.

Alitoa maagizo hayo jana mkoani hapa, baada ya kukagua ujenzi wa sekondari hiyo na kukuta kasoro nyingi ikiwamo ubovu katika madawati, vyumba vya maabara na bwalo la wanafunzi, ukosefu wa nyavu za kuzuia mbu, wakati serikali ilishalipa Shilingi bilioni tatu za kukamilisha majengo yote ya shule hiyo.

Pia, aliagiza Mkurugenzi Mtendaji mstaafu, Lain Ephraim Kamendu, ahojiwe pamoja na wenzake kuhusu matumizi mabaya ya fedha hizo.

Katika ukaguzi wa bwalo, Majaliwa alielezwa na mhandisi Sagachuma kwamba bwalo hilo lilitengewa Sh. milioni 774 na wameshatumia Sh. milioni 341 hadi kufikia hatua ya lenta ambayo alidai ni sawa na asilimia 40 ya ujenzi wake.

Hata hivyo, Majaliwa alipouliza fedha za ujenzi zilizobaki ziko wapi, mhandisi huyo alijibu kwamba hazipo, hata Ofisa Elimu Sekondari naye alishindwa kutoa ufafanuzi.

"Unasema utajenga kwa chuma hapa juu, hizo nondo ziko wapi? Mabati yako wapi? Majiko yako wapi? Hapa tunatarajia kuwa na watoto 172, je watakula wapi hawa na masomo yameshaanza?" Alihoji Majaliwa.

"Wewe ni Ofisa Elimu na kazi yako ni kusimamia ujenzi wa shule zote, ni kwa nini hukutoa taarifa ya kusuasua kwa ujenzi kwenye Kamati ya Ulinzi ya wilaya yako? Taarifa nilizonazo ni kwamba mkurugenzi aliyekuwapo alikuwa anakupangia kazi kwenye vituo vya mbali ili usije hapa, lakini bado ulikuwa na wajibu wa kutoa taarifa juu ya mwenendo huo."

Aidha, Majaliwa alimhoji mhandisi huyo kwa nini mifereji ya kupitisha gesi na maji machafu katika maabara imezibwa yote, lakini hakupewa majibu ya kutosheleza.

"Mifereji haina vishikio, wamejaza matofali hata mwalimu akitaka kukagua mifumo ya gesi au mifereji ya maji machafu hawezi kuinua hilo tofali. Mifuniko ya mifereji inayopitisha maji, bomba za umeme na gesi kwenye maabara ya shule hiyo itolewe na irekebishwe upya," alisema.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Joachim Nyingo, kusimamia mchakato wa kurudisha madawati yaliyoletwa ambayo ni mabovu kwa gharama za mkandarasi, yaletwe mengine mapya.

"Nimeagiza fundi aliyejenga madirisha atafutwe, aletwe ili aweke nyavu kwenye jengo la utawala. Aliyetengeneza madawati aitwe akayatengeneze upya kwa viwango vinavyotakiwa na kwa gharama zake," alisema Majaliwa.

Vilevile, alimuagiza Kamanda wa TAKUKURU, Mkoa wa Iringa, awahoji watumishi hao na aanze uchunguzi haraka.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akisaga nafaka kwa kutumia mawe kama ilivyokuwa miaka ya nyuma enzi za mababu zetu, kwenye tamasha la utamaduni wa kabila la wasukuma Sanjo ya Busiya katika Ikulu ya Chifu Makwaia kijiji cha Negezi wilayani Kishapu lililoandaliwa na mjukuu wake Chifu Edward Makwaia kwa lengo la kuenzi mila na desturi za kabila la wasukuma lililohitimishwa juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## INEC yawaita wananchi kuboresha taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imewataka wananchi na wapigakura mkoani Katavi kujitokeza kwa wingi kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Akifungua mkutano wa wadau wa uchaguzi mkoani Katavi, Mjumbe wa INEC, Asina Omari, alisema maboresho hayo yatafanyika Julai 20 hadi 26, mwaka huu, na kwamba kufanikiwa kwake kunategemea ushirikiano wa wadau wa uchaguzi katika kuwahamasisha wananchi.

"Tume inatarajia kupata ushirikiano mkubwa zaidi kutoka kwenu, kwa kuwafikishia wananchi wa Mkoa wa Katavi taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu zoezi lililopo mbele yetu la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura na kuwahamasisha wananchi wenye sifa ya kujiandikisha kuwa wapigakura, wajitokeze kwa wingi kwa tarehe ambazo Tume imeziweka kwa kila kituo," alisema.

Asina ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu, aliwapongeza wananchi na wadau wa uchaguzi mkoani humo kwa kuwa miongoni mwa mikoa ya mwanzo kufikiwa na maboresho hayo.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano huo, Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura, Giveness Aswile, alisema uzinduzi wa uboreshaji utafanyika mkoani Kigoma Julai 20, 2024 na utaanza siku hiyo kwenye mkoa huo na mikoa ya Katavi na Tabora.

"Siku ya uzinduzi ndiyo siku ambayo pia uboreshaji utaanza katika Mkoa wa Kigoma sambamba na mkoa huu wa Katavi na Tabora na kufuatiwa na Kagera na Geita," alisema.

Aidha, alisema lengo ni kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, uboreshaji kwa awamu ya kwanza utafanyika kwenye mizunguko 13 itakayobainishwa kwenye ratiba.

"Zoezi hili litaendeshwa kwa siku saba kwenye kila kituo cha kuandikisha wapiga kura. Tunatarajia zoezi litakamilika Machi, 2025," alisema.

# Makonda: Nitajieni wanaokwamisha kesi za ubakaji, ulawiti

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amewataka wananchi wenye kero au kesi za ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji na ulawiti kufika ofisini kwake Julai 12, mwaka huu, ili kubaini anayekwamisha kupatikana haki.

Akizungumza na wadau wa mashirika na asasi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na huduma za jamii, jijini hapa jana baada ya kuibua hoja mbalimbali za matukio ya ulawiti na ubakaji bila kuchukuliwa hatua.

Alisema lengo la kukutana na kundi hilo ni kujua kwanini kesi hizo zinakwama na anayezikwamisha, kwa ajili ya kuwezesha watuhumiwa kufikishwa mahakamani na haki kupatikana kwa pande zote.

Alisema matukio ya ubakaji na ulawiti yamekuwa kero kubwa mkoani humo, na kwamba kuna baadhi ya wazazi na walezi hawawajibiki ipasavyo kutokana na wazazi kuwa makini zaidi kutafuta fedha na kuwaachia jukumu la malezi watu wengine.

Alisema utafiti wa awali umebaini kuwa baadhi ya watoto wanalawitiwa na kubakwa kutokana na uangalizi hafifu.

"Hizi kesi za ubakaji na ulawiti zinasikitisha sana, lakini lazima tutafute kiini chake na kuna kesi moja nimeisikiliza na Mkurugenzi wa Husna Foundation, Husna Almasy, ametupa uelewa kuwa mama mzazi wa mtoto huyo anajua vema aliyemlawiti mtoto wake, lakini anatumia mbinu ya kusingizia watoto wengine kumbe mhusika mkuu anamjua," alisema Makonda na kuongeza:

"Mimi RC Makonda ni mpole kuliko watu wengine duniani, lakini katika jambo la ulawiti na ubakaji, nitachukua hatua katika hili tukio la mtoto wa miaka mitatu wa kiume kufanyiwa ukatili huku mzazi wa mtoto huyo akificha ukweli wa tukio zima, ila ikithibitika huyu mama anajinufaisha na tukio hili asije kunilaumu."

Makonda aliwataka wazazi na walezi kusimama imara kulinda watoto wasifanyiwe ukatili ikiwamo utoaji wa taarifa, ili kufanyiwa kazi na haki ipatikane, maadili yanazingatiwa na ulinzi wa watoto ni jukumu la kila mmoja.

Aliagiza watu wote waliofanyiwa ukatili kwa watoto kubakwa au kulawitiwa na kesi zao hazijulikani zimeishia wapi, wafike ofisini kwake Alhamisi (keshokutwa) ili kusema ukweli na kujua zimekwama wapi.

Awali, Husna alidai tukio la mtoto wa miaka mitatu kudaiwa kulawitiwa na watoto wenzie jijini Arusha, limetendwa na mtu mzima.

Alisema ukweli wa tukio hilo anajua mama mzazi wa mtoto huyo kwa kuwa vipimo vya daktari vinaonesha aliyefanya tukio hilo ni mtu mzima.

"Watoto walikamatwa na kupelekwa kituo cha Polisi Murriet, uhalisia wa tukio hilo mama mzazi wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa) anajua, aliyefanya tukio la ulawiti wa mtoto huyo anamjua hataki kueleza ukweli badala yake anasingizia watoto wanaoishi mitaani," alisema.

## Kaya 11 Kilimanjaro zanusurika nyumba zikiteketea moto

**Na Godfrey Mushi**, SIHA

KAYA 11 zenye wakazi 18 katika Kijiji cha Ngarenairobi, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wamenusurika kifo baada ya jiko la gesi kulipuka na kuteketeza makazi yao.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji hicho (VEO), Seif Mwemgamba, tukio hilo lilitokea Julai 6, saa 1:30 usiku.

"Huo moto ulitokea katika chumba kimoja cha mpangaji wa jengo hilo linalokaliwa na kaya hizo, na kibaya zaidi limejengwa kwa asilimia 80 kwa mbao.

"Hasara iliyojitokeza ni kubwa, kwa sababu wananchi wamepoteza kila kitu kilichokuwa ndani. Hivi sasa wanahitaji misaada ya kibinadamu, kama magodoro, chakula na mavazi.

Ofisa Mtendaji huyo alisema kutokana na janga la moto kutokea mara kwa mara katika eneo hilo, wananchi wamekuwa wazito kubadili kujenga nyumba za kisasa, hasa za tofali na kuishia kujenga nyumba za mbao.

Wiki tatu zilizopita, katika kijiji hicho cha Ngarenairobi, nyumba nyingine iliteketea kwa moto na kuacha kaya moja bila makazi.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Christopher Timbuka, alisema kinachowaumiza kichwa viongozi kwa sasa ni mahali pa kuwahifadhi wananchi hao ambao wamebaki bila makazi.

# CCM yaahidi kusimamisha wagombea chaguo la wananchi

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema katika uchaguzi mkuu mwakani kitasimamisha wagombea chaguo la wananchi na wasiokuwa na makandokando.

Uamuzi huo unatokana na fundisho kwamba mgombea anayekataliwa na kisha chama kikampeleka anakuwa sio matakwa ya wananchi.

Katibu wa NEC, Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, alitoa ahadi hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Chanika, Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya siku saba mkoani humo.



Alisema ni muhimu viongozi wakawajibika kwenye nafasi zao kutatua kero za wananchi.

Kwa mujibu wa Makalla, kero zilizoibuliwa na wananchi wa eneo hilo ni wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kutozwa fedha wanapohudhuria kliniki na kero ya mfumo mbovu wa uchomaji taka unaochangia moshi kuzagaa kwenye makazi ya wananchi wanaoishi jirani na Hospitali ya Nguvu Kazi, Chanika.

Kuhusu wagombea, Makalla alisema, "Tumeshaelezana Halmashauri Kuu za wilaya msibebe wagombea ambao siku mnamweka tu watu wanaanza kuguna.

"Tunaahidi tutawaletea wagombea wazuri, safi na wanaokubalika ambao watawatumikia wananchi."

Kuhusu Hospitali ya Nguvu Kazi, kuwa kati ya kero 26 zilizotolewa na wananchi, Makalla alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Zaituni Hamza, kufuatilia jambo hilo ikiwamo matumizi ya lugha mbaya kwa wagonjwa kunakofanywa na watumishi.

Aidha, alimwagiza Mganga Mkuu kuhakikisha suala hilo halijirudii na katika Kituo cha Afya cha Kinyerezi ambacho amekitembelea na kuona namna kinavyohudumia wananchi.

Zaituni aliwaeleza wananchi kuwa tayari amewasiliana na uongozi wa hospitali hiyo kuhusu changamoto zilizoelezwa na kuahidi jana angerudi kuzishughulikia.

Jana katika Kituo Afya cha Kinyerezi, Makalla alisema uamuzi wa serikali kukipandisha hadhi kituo hicho kumesaidia wakazi wa Segerea kupata huduma nzuri.

Wananchi pia waliibua kero za huduma muhimu maeneo ya ardhi, uunganishaji umeme na barabara ambazo, Makalla alimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, kuzishughulikia.

Aidha, kero zinazohusu ardhi alimkabidhi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, akimtaka kuzitatua kwa haraka ikiwamo mpaka wa Kazimzungwi.

Makalla alisema chama kitaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kero za wananchi zinapatiwa ufumbuzi.

Viongozi hao wa CCM walitembelea Shule ya Sekondari Minazi Mirefu, Ukonga yenye madarasa 20 na matundu ya vyoo 45 ambao ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 90 na itawekewa mfumo wa lifti.

Juzi katika mkutano wa hadhara, Mbunge wa Ukonga, Silaa alitumia mstari wa biblia Mathayo 21:12-13 ambao unasema Yesu aliingia hekaluni kuondoa wanyang'aji akimuomba Makalla amfikishie salamu Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwamba, aingie katika ofisi za vijiji, vitongoji na mitaa zilizogeuzwa mapango ya wanyang'anyi wa ardhi akapindue meza na kurudisha tumaini kwa Watanzania ili wapate watu wasafi watakaomsaidia Rais kulinda maslahi ya taifa.

Mkuu wa Kitengo cha Burudani na Hamasa CCM, Upendo Peneza, alisisitiza Watanzania kuwachagua wagombea wa CCM kwa kuwa ndio wanaofaa.

Alisema Rais Samia amejenga nchi ya kidemokrasia na kuondoa zuio la kufanya mikutano ya kisiasa na kuwakaribisha wapinzani mezani ili kuwa na nchi yenye maelewano.

"Wakati Rais ametoa neema hiyo, amefuata Katiba, badala yake watu tuliowategemea waikosoe serikali leo ndio wanatutuhumiana rushwa, hawaaminiki tena," alisema Peneza.

# Wadau: Waandishi wa habari wafunzwe kwa vitendo vyuoni

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa habari wamesema mzizi wa tatizo la wahitimu wa sekta hiyo kutoiva vyema ni kutofanya mafunzo ya vitendo na kukosekana kwa wakufunzi wenye taaluma hiyo na badala yake kutumika nadharia kama inavyofanyika sasa.

Aidha, wamesema baadhi ya vyuo vina wanafunzi wengi kuliko uwezo wa rasilimali watu (wakufunzi) na vitendea kazi, huku wengine wakitupia lawama vyombo vya habari kuwapa alama za juu wanafunzi licha ya kutofanya vizuri kwenye mafunzo ya vitendo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wataalamu wa sekta ya habari, walisema matokeo na mapendekezo ya utafiti uliofanywa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), kuhusu hali ya vyombo vya habari nchini yamegusa maeneo muhimu na lazima hatua madhubuti zichukuliwe.

Mhadhiri katika Shule ya Uandishi wa Habari, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), Dk. Abdallah Katunzi, alisema anakubaliana na kilichoelezewa katika utafiti huo, kuwa ni malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wadau mbalimbali.

Alisema hali hiyo inatokana na mitaala katika vyuo vikuu kujikita katika nadharia zaidi kuliko vitendo na kuwa vigumu kuzalisha watu waliobobea kwenye utendaji kazi.

Alitaja pia sababu nyingine ni vyuo hasa vya serikali kutokuwa na vifaa vya kufundishia vya kisasa vinavyoendana na soko kama vile kamera, kompyuta na virekodia sauti.

"Sasa mwanafunzi asijifunze kwa kutumia kifaa kilichotengenezwa mwaka 2000 wakati sokoni kuna kifaa cha mwaka 2023. Sasa kuna upungufu wa hivi vifaa," alisema.

Sababu nyingine ni wanafunzi wanaokwenda katika vyuo hivyo kutokuwa na msingi mzuri wa masomo ngazi ya msingi hadi sekondari na kuwa vigumu kujifunza katika ngazi ya chuo kikuu.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Neema, alitupia lawama vyumba vya habari kuwa havitilii maanani mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi hao kwa kuwa vinawapa alama za juu.

"Hawa wanafunzi wanapotoka kwenye vyumba vya habari wahariri wanawapa alama 'A', sasa inakuwaje wakija kuanza kazi wanalalamikiwa kuwa hawajui kitu," alihoji.

Josephine Christopher aliyemaliza masomo SJMC miaka miwili iliyopita, alisema kuwa masomo ya kupiga picha na kuchukua video yalikuwa magumu kwake kwa sababu yalikuwa yanafundishwa kwa nadharia.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Tawi la Dar es Salaam, Pristus Silayo, alisema anachokutana nacho chuoni kwa sasa ni walimu kufundisha zaidi nadharia kuliko vitendo akijiona kuwa anakuwa mbobezi kwenye nadharia zaidi ya vitendo.

Alitoa mfano kuwa baadhi ya vyuo hakuna magazeti, wala redio wala vipindi vya luninga vya wanafunzi kujifunzia au kuyatekeleza mafunzo yao kwa vitendo, huku walimu wakitegemea kuwa mwanafunzi akitoka hapo atakuwa mbobezi kwa kile alichojifunza.

**NINI KIFANYIKE**

Dk. Katunzi amevishauri vyombo vya habari kuanzisha utaratibu wa kuwalea wanafunzi waliomaliza vyuo na kuingia kwenye vyumba vya habari, ili wajue utaratibu wa vyumba hivyo na kufanya kazi kwa weledi.

"Sasa tukisema vyuo vifanye kila kitu halafu vyumba vya habari vikajitoa hatutoweza kupata mtu bora, kwa hiyo hata kama tutaweka mitaala mipya ukapata na walimu wazuri bado nafasi ya vyumba hivyo katika kuwalea watu hao ipo palepale," alisisitiza.

Aidha, aliwashauri wamiliki wa vyuo vikuu binafsi kudahili wanafunzi wenye uwezo wa kuwafundisha kulingana na rasilimali watu na vitendea kazi walivyonavyo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Kampasi ya Dar es Salaam, Padri Dk. Francis Ngatingwa, alisema ni muhimu vyuo vya uandishi wa habari kuwa na maabara za kuwafundisha wanafunzi kwa vitendo badala ya kutegemea kuwapeleka kwenye vyombo vya habari kujifunza.

Alisema hali hiyo inawapa uwanda mpana wanafunzi kujifunza kwa vitendo hata wanapokwenda kwenye vyumba vya habari kufanya mafunzo kwa vitendo wanakuwa wanajua nini cha kufanya.

Alishauri wapewe muda wa kutosha wa kujifunza kwa vitendo kwenye vyombo vya habari, akishauri wakae huko kuanzia miezi mitatu na kuendelea badala ya utaratibu ulipo sasa wa kukaa wiki nne.

Meena alishauri vyombo vya habari kuwatengenezea mfumo mzuri wanafunzi hao wanapokwenda kwenye mafunzo ya vitendo, ili wanapomaliza alama wanazowawekea ziendene na utendaji kazi wao.

Mhadhiri na Mratibu wa Taaluma SJMC, Dk. Gidion Kamfipo, alisema kuwa kwa sasa wanaboresha mitaala ya kufundishia katika shule hiyo ili iendane na hitaji la soko na maendeleo ya teknolojia katika tasnia ya habari.

Alisema uboreshaji huo unajikita katika stadi na ujuzi ili mwanafunzi akimaliza chuo awe na uwezo wa kwenda kufanya kazi moja kwa moja, pia wanaagalia masuala mtambuka yaliyojitokeza kama vile ujumuishaji wa jinsia na makundi maalum.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Soko limepatikana ni wakati wa kuchangamkia kilimo cha parachichi

**MATUNDA** ya parachichi yametokea kupendwa na soko lake ni kubwa duniani kutokana na faida zinazopatikana kutoka kwenye tunda hilo.

Kwa Tanzania tumebahatika kuwa na mikoa ambayo zao hilo linastawi vizuri na utafiti unaonesha kuwa parachichi kutoka nchini kwetu lina ubora kulinganisha na nchi zingine zinazozalisha tunda hilo.

Mwishoni mwa wiki Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwahimiza wananchi wa mkoa wa Iringa na Watanzania kwa ujumla waingie kwenye kilimo cha matunda hayo kwa kuwa zao hilo linachochea ukuaji wa uchumi.

Serikali imefanya juhudi katika kipindi cha miaka mitatu, kutafuta masoko kwa ajili ya maparachichi yanayozalishwa nchini badala ya kutegemea nchi jirani pekee.

Nchi ambazo kuna soko la uhakika ni China na India kutokana na thamani kubwa na ubora wa hali ya juu ya maparachichi yanayozalishwa Tanzania ukilinganisha na kutoka nchi nyingine.

Watanzania wametakiwa kuingia kwenye mpango wa kuzalisha miche ya zao hilo ili kuongeza idadi ya uzalishaji wa maparachichi. Hiyo ni kutokana na ubora mkubwa. Na hii ni baada ya kupima udongo nchini kote na kubaini kuwa Tanzania ina maeneo yenye udongo unaofaa kwa kilimo hicho.

Pamoja na kuhimiza kilimo hicho, pia suala la miundombinu ya barabara lazima lizingatiwe ili matunda hayo yatakapofikia msimu wa mavumo yasiozee mashambani kwa kushindwa kusafirishwa kwasababu ya ubovu wa barabara.

Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) pamoja na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), wana jukumu kubwa la kuhakikisha miundombinu ya barabara inapitika vizuri.

Tanzania ina Baraka ya kupata ardhi nzuri ya mazao na mavuno mengi, lakini tatizo kubwa ni usafirishaji wa mazao kwenda sokoni kutokana na barabara mbovu ambazo wakati wa mvua ndio hali huwa mbaya zaidi. Tatizo hilo husababisha wakulima kupata hasara kutokana na mazao mengi kuozea kwenye maghala au mashambani kwa ugumu wa kusafirishwa.

Hivyo ni muhimu wakati wananchi wanahamasishwa kilimo hicho, iendane sambamba na kasi ya utengenezaji wa miundombinu ya kusafirisha mazao hayo.

Pia, wananchi wapewe elimu ya kutokubali wafanyabiashara wanaokwenda kuwarubuni kwa kununua mazao yakiwa hayajakomaa na kuuza kwa bei ya chini.

Ni habari njema kutoka kwa Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, kuwa serikali imeshasaini mkataba na kampuni ya Afac Engineering ambayo itajenga kiwanda cha kusindika maparachichi katika eneo la Nyololo ambapo katika awamu ya kwanza, Sh. bilioni 3.4 zitatumika.


"Wana-Mufindi ni watu wanaolima sana. Mbunge wenu amesimamia ahadi ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kujenga kiwanda cha kusindika maparachichi. Mkataba ulisainiwa na kabla ya Ijumaa ijayo, tutamkabidhi eneo mkandarasi ili aanze kazi."

Kujengwa kwa viwanda vya kuchakata matunda ni njia nzuri ya kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini badala ya kuuza ghafi.

Wanunuzi wa bidhaa zetu ghafi huenda kuzichakata na kuja kuziua nchini kwetu kwa bei za juu, hali inayokosa mapato nchi.

Ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao utasaidia pia, kuokoa yanayooza shambani kwa kuongezewa thamani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Chanzo wingi ajali bodaboda kijulikane

**MAJERUHI** 163,148 wa ajali za barabarani, walipokelewa katika vituo vya huduma za afya katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Dodoma na Kagera, ambayo ni maeneo vinara wa ajali .

Aidha, majeruhi 11,434 walihudumiwa kwenye hospitali 16 za rufaa katika kipindi cha kuanzia Juni 2023 hadi Juni mwaka huu, huku wale wa bodaboda wakiwa ni asilimia 61 ya majeruhi wote.

Hayo ni kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dk. John Jingu ,wakati akizungumza katika semina na wadau wa usafirishaji inayofanyika jijini Dodoma hivi karibuni.

Katika semina hiyo, katibu mkuu anawapa jukumu wadau hao, hasa madereva kuwa vinara wa kudhibiti ajali za barabarani ili kuokoa nguvu kazi ya taifa inayoteketea kwa ajali.

Ninadhani umefika wakati wa kutafuta chanzo cha ajali hizo, kwani kama ni elimu, imekuwa ikitolewa mara kwa mara, lakini pia inaelezwa kuwa kwenye udereva wa bodaboda wamo pia wasomi.

Sasa kama wamo wasomi, wanakwama wapi kuzingatia kile ambacho wanafundishwa na kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria ya usalama barabarani ili wawe salama na abiria wao?

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limekuwa likikaa na madereva wa bodaboda vijiweni na kuwapa elimu, limekuwa likifanya hivyo mara kwa mara, lakini tatizo bado linaendelea.

Ninadhani ni vyema sasa chanzo cha wingi wa ajali za bodaboda kikaendelea kutafutwa ili kujua wanakwama wapi hadi wanajikuta wakisababisha ajali mara kwa mara na kupoteza maisha.

Katika mazingira hayo, wapo wengine wanapata ulemavu wa kudumu na kujikuta wakishindwa kufanya shughuli zao za kila siku na kubaki kutegemea watu wengine maisha yao yote.

Pamoja na hayo, madereva wenyewe wanaweza kujiongeza kwa kuepuka tabia hatarishi kama kupita kwenye makutano ya barabara kabla ya kuruhusiwa na taa, 'kuovateki' kushoto, kubeba abiria juu ya mizigo au zaidi ya mmoja, kutovaa kofia ngumu na kuwa na haraka kila wakati.

Vilevile wanaweza kuacha kuendesha mwendo wa haraka hata katika barabara za mitaani na kutosimama kwenye alama za pundamilia au kuacha kupita pembeni mwa barabara kwa kukwepa matuta.

Madereva hao pia wanaweza kuacha kuendesha kwa haraka katika njia ya waenda kwa miguu au kuacha kuendesha wakiwa wamelewa, kwani baadhi yao wamekuwa wakituhumiwa kuendesha wakiwa wamelewa.

Kwa ujumla ni kwamba, zipo tabia nyingi hatarishi ambazo wakiziacha, usafiri wa bodaboda unawezaa kuwa salama kwao, kwa abiria wao na hata kwa waenda kwa miguu.

Inasikitisha kusikia kwamba, kwa mwezi Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), inapokea majeruhi 700 wa ajali huku asilimia 60 wakiwa wamejeruhiwa kutokana na ajali za bodaboda.

Idadi hiyo inatajwa kuwa ni sawa na wastani wa majeruhi 23 wa ajali kila siku, huku ajali hizo zikiwapata madereva wa bodoboda wenyewe, abiria au watembea kwa miguu wanaogongwa.

Binafsi njia nzuri ninayoiona ni kuendelea kuwapa elimu ihusuyo usalama barabara, lakini pia wale wasioizingatia, washurutishwe ili wawe salama na abiria au waenda kwa miguu.

Wasipuuzie elimu ambayo inatolewa kwao na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kwani ndio inayoweza kuwaweka salama iwapo wataizingatia.

Ni kweli kwamba ajali haina kinga, lakini kwa jinsi wanavyoendesha vyombo hivyo bila kuzingatia sheria ya usalama barabarani, ni wazi ajali nyingine huwa wanazisababisha kwa kutokuwa makini barabarani.

Kwa mfano, wanazuiwa kubeba abiria zaidi ya mmoja, lakini wanabeba, wanafika makutano ya barabara, badala ya kusubiri taa ziwaruhusu, wao wanavizia ili wapite kabla na bila kuruhusiwa na taa.

Tabia hiyo inaweza kusababisha ajali, kwani chombo cha moto kinaharibika wakati wowote na kama dereva atakuwa amevizia ili kuvuka bila kuruhusiwa, anaweza kujikuta akiharibikiwa katikati ya barabara na hata kugongwa na magari kutoka upande ambao umeruhusiwa kupita.

HABARI KITAIFA

## Atoa ushuhuda kupata haki baada ya miaka 16

**Na Elizabeth Zaya**

YUNUS Milingani, mkazi wa Dar es Salaam ametoa ushuhuda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, alivyoteseka kwa miaka 16 akitafuta haki ya ardhi yake aliyodhulumiwa.

Ushuhuda huo aliutoa jana katika banda la msaada wa kisheria la Mama Samia kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kiamatifa ya Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea katika Barabara ya Kilwa, Temeke.

Alisema ardhi aliyodhulumiwa ni mashamba mawili tangu mwaka 2009 na kila anapotafuta haki amekuwa akikumbana na vikwazo vinavyokwamisha kupata haki yake.

"Kwa dhati kabisa ya moyo wangu, naona jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kwa raia wake, anajitahidi kwa kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao kwa msingi kwamba haki inainua taifa na dhuluma inaangamiza taifa, nimeshukuru kwa hilo.

"Kwa hiyo tunaomba na wale wanaosimamia na kuitekeleza kama majaji na mahakimu nao watende haki kama ilivyo dhamira ya Rais Samia, wasimwangushe, tunaona ameleta mpaka kampeni hii inayosaidia wananchi kutatua migogoro kisheria, kwa maana hiyo hapendi kuona dhuluma inafanyika, anataka watu wapate haki," alisema Milinga.

Alisimulia kuwa, mwaka huu, moja kati ya mashamba yake mawili limeamuliwa mwaka huu na jingine bado.

"Nilikuwa na shida ya maeneo yangu mawili ya mashamba, nilifanyiwa dhuluma, moja tangu mwaka 2009, lakini kesi imekwenda mpaka mwaka huu ndio ikahukumiwa, yaani mtoto anaanza darasa la kwanza mpaka anahitimu kidato cha nne kesi haijaisha, lakini tunamshukuru mama Samia kwa kuweka juhudi zake na timu yake kutusaidia.

Matarajio yangu yamekuwa makubwa sana, nimefarijika, nimefurahi, Mungu ampe uhai mrefu."

Akizungumza baada ya kutoa huduma ya kisheria kwa mzee huyo, Katibu Mkuu Makondo, aliahidi kufuatilia suala la mwananchi huyo pamoja na nyingine zote ambazo wamezipokea katika maaonesho hayo na kuhakikisha haki inatendeka.

"Nimefika hapa sabasaba, nimezungumza na Yunus Milinga ambaye ana changamoto ya uvamizi wa maeneo yake mawili, moja inahusiana na kesi ambayo imeshahukumiwa mwaka huu na Baraza la Ardhi na nyumba la wilaya na amepata haki, lakini jingine bado, sisi wizara kupitia kampeni hii tunalichukua, tutafuatilia kuhakikisha kwamba haki inapatikana," alisema Makondo.

"Kwanza linahitaji uchunguzi kwa sababu kuna masuala ambayo yatahitaji kuthibitishwa na yakishathibitishwa yatampatia haki katika eneo jingine.

Kwa hiyo tunawasihi wananchi wazidi kujitokeza kwa wingi kwa sababu huduma hizi ni bure, tunawapatia elimu kuhusiana na Katiba, sheria ya nchi na tunatatua kero zao moja kwa moja hatuweki 'pending' (pembeni)."

Makondo alisema kati ya migogoro wanayopokea kupitia kampeni hiyo ya Mama Samia Legal Aid Campaign ni pamoja na yale yanayohusiana na jinai.

"Yapo masuala ambayo yanajitokeza katika kampeni hii ambayo mengine yanahusiana na jinai ambayo tutashirikiana na vyombo mahususi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba haki inaonekana inatendeka kwa wananchi," alisema Makondo.



Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba (Kulia), akiagana na Balozi wa Denmark nchini Tanzania aliyemaliza muda wake, Mette Dissing-Spandet, baada ya kikao chao kilichofanyika katika Ofisi za Hazina Ndogo, jijini Dar es Salaam, ambapo ameiomba Denmark kuongeza ushirikiano katika sekta za nishati, maendeleo ya sekta ya fedha na kukuza uwekezaji, katika mpango wao mpya wa ushirikiano wa kimataifa unaoandaliwa na nchi hiyo. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Waziri Makamba: Tanzania yajizatiti kuimarisha EAC

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba amesema Tanzania imejizatiti kuhakikisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inakuwa imara, yenye umoja na inayofikia malengo yake.

Akiongoza mkutano wa faragha wa siku tatu wa mawaziri wa mambo ya nje na wanaoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Makamba alisema madhumuni ya mkutano huo ni kuwa na familia imara, kuiwezesha Jumuiya hiyo kutekeleza majukumu yake vizuri.

Alisema Tanzania kama moja ya nchi waanzilishi wa Jumuiya hiyo imejizatiti kuiona ikiwa na umoja, imara na yenye kufanikisha mipango na malengo yake.

Alisema kufanyika kwa mkutano huo kunatokana na maelekezo ya wakuu wa nchi na kuongeza kuwa ni matarajio ya Tanzania kuwa viongozi hao watazungumza kiungwana, kwa uwazi kwa lengo la kuimarisha Jumuiya.

"Umoja ndio nguvu yetu, tumeona katika siku za nyuma tulipojaribu kuwa na umoja huu, lakini ukavunjika, madhara ya kuvunjika kwa umoja ule bado tunayo na kwa hali hiyo hatupaswi kurudia tena makosa hayo," alibainisha Makamba.

Akizungumza katika kikao hicho, Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kenya, Musalia Mudavadi, aliipongeza Tanzania kwa kukubali kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kuongeza kuwa ni wakati mwafaka kwa nchi wanachama kutumia fursa mbalimbali ndani ya jumuiya kwa manufaa ya wananchi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Afrika Mashariki wa Jamhuri ya Uganda, Rebecca Kadaga, aliishukuru serikali ya Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kupongeza juhudi za kuimarisha jumuiya ambazo zimeoneshwa kuchukuliwa na viongozi wakuu.

Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la EAC, Dend Alor Kuol, alisema kufanyika kwa mkutano huo ni jambo jema hasa ikizingatiwa kuwa unaangalia masuala ya amani, usalama na mtangamano wa jumuiya ikiwa ni hatua maridhawa katika kuifanya jumuiya kusonga mbele.

Mkutano huo wa faragha unajadili taarifa ya Mwenyekiti wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya; hali ya amani, usalama, siasa na uhusiano kati ya nchi wanachama; unatathmini na kujadili mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na masuala yanayokwamisha ufikiwaji wa malengo ya programu na miradi inayojiwekea.

Mkutano huo umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao Mei 7, mwaka huu.

Mawaziri kutoka nchi nane wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zikiwamo Burundi, DRC, Kenya, Rwanda, Somalia, Sudan Kusini, Uganda na Mwenyeji Tanzania wanahudhuria mkutano huo pamoja na makatibu wakuu kutoka katika wizara hizo na wajumbe wa Sekretarieti ya EAC.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# PM ahamasisha kilimo cha parachichi kuchochea uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka wana-Iringa na Watanzania kwa ujumla waingie kwenye kilimo cha parachichi kwa kuwa zao hilo linachochea ukuaji wa uchumi.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, serikali ilikuwa ikitafuta masoko kwa ajili ya maparachichi yanayozalishwa nchini badala ya kutegemea nchi jirani pekee.

"Tumeshapata soko la moja kwa moja kwa ajili ya maparachichi yetu nchini China na India na tumegundua ya kwetu yana thamani kubwa na ubora wa hali ya juu ukilinganisha na maparachichi kutoka nchi nyingine."

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi na viongozi mbalimbali baada ya kukagua mradi wa kitalu cha miche bora ya parachichi unaomilikiwa na kikundi cha vijana cha Chilongola, kata ya Upendo, Mafinga Mjini, mkoani Iringa.

Aliwataka Watanzania waingie kwenye mpango wa kuzalisha miche ya zao hilo ili kuongeza idadi ya uzalishaji wa maparachichi. "Maparachichi yetu

yana ubora mkubwa. Na hii ni baada ya kupima udongo nchini kote na kubaini kuwa tuna maeneo yenye udongo unaofaa kwa kilimo hiki," alisema.

Akizungumzia suala la barabara kama lilivyowasilishwa na wana kikundi hao, Waziri Mkuu alisema miundombinu ya barabara za kwenda mashambani linaratibiwa vizuri na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) pamoja na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS).

Kuhusu suala la kukosa mlango wa malimbichi bandarini, alisema analipokea na kuahidi kuwa atalifuatilia.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema serikali imeshasaini mkataba na kampuni ya Afac Engineering ambayo itajenga kiwanda cha kusindika maparachichi katika eneo la Nyololo na katika awamu ya kwanza, Sh. bilioni 3.4 zitatumika.

"Wana-Mufindi ni watu wanaolima sana. Mbunge wenu amesimamia ahadi ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kujenga kiwanda cha kusindika maparachichi. Mkataba ulisainiwa na kabla ya Ijumaa ijayo, tutamkabidhi eneo mkandarasi ili aanze kazi," alisema.

Kuhusu kusuasua kwa zao la chai, alisema serikali

inatambua changamoto katika kiwanda cha DL, lakini imeshafanya uamuzi wa kukinunua kiwanda hicho na kukikabidhi kwa wakulima wadogo wa chai wa Mufindi ili wakiendeshe kupitia ushirika wao.

Kuhusu soko la mahindi, Silinde aliwataka wananchi hao wajiandae kuuza mahindi kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuanzia Julai 10, mwaka huu na kuahidi kuwa bei itakuwa nzuri. Hata hivyo, hakutaja bei hiyo.

Akifafanua zaidi, alisema: "Kutoka Zambia, tumepokea oda ya tani 650,000 za mahindi. Nchi jirani ya Congo (DRC) nao wametaka tani 500,000, lakini wanataka tuwape tani 200,000 za awali. Kwa hiyo, jiandaeni kuuza mahindi kuanzia tarehe 10 Julai, 2024."

Mkurugeni wa kampuni ya Chilongola Agroforestry & Livestock, Andrew Salika, alisema kikundi chao kilianza mwaka 2020 kwa kuzalisha miche 9,000 na sasa wana miche 250,000 iliyo tayari kwenda sokoni. "Lengo letu ni kuongeza idadi ya miche bora ambapo mahitaji ni miche 730,000 kwa msimu mmoja," alisema.

Mbunge wa Mafinga Mjini, Cosato Chumi alisema mji wa Mafinga ni

miongoni mwa iliyo kwenye mradi mkubwa wa maji wa miji 28 nchini, lakini umefikia asilimia 18 pekee kutokana na kusuasua kwa kasi ya mkandarasi.

Aliiomba serikali isimamie kwa karibu ujenzi wa barabara ya Mafinga hadi Mgololo kwa kuwa Wilaya ya Mufindi inabeba uchumi wa mkoa mzima wa Iringa. "Barabara hii ikiisha, itarahisisha sana usafirishaji wa mazao ya wakulima na kuwa mkombozi wa wananchi wengi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Dkt. Linda Salekwa, alimweleza Waziri Mkuu kwamba wilaya hiyo ina ekari 800,000 ambazo ni miti pekee na kati ya hizo, 500,000 ni za miti ya kupandwa. Alisema wilaya hiyo ina viwanda 40 vya kuchakata mazao ya miti pamoja na mazao ya kilimo kama chai na pareto.



Mjumbe wa Kamati ya Rufaa, Said Miraji(kulia) akizungumza katika Mkutano wa Kamati ya Rufaa wa Chama cha Alliance for Democratic Change-ADC Dar es Salaam jana, ambapo kamati hii inatarajia kutoa majibu kuhusu malalamiko ya uchaguzi wa nafasi ya Uenyekiti uliofanyika mwezi uliopita. Wa pili kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Lydia Bendera, wa pili kushoto ni Katibu wa Kamati hiyo, John Mbogo na aliyekuwa mgombea nafasi ya Uenyekiti wa chama hicho ambaye pia ni mlalamikaji, Doyo Hassan. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Makinda ashauri Sensa itumike kupanga mipango

**Na Elizabeth Zaya**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka mwaka 2022, Anna Makinda, amewataka Watanzania kutumia takwimu za sensa kupanga mipango mbalimbali.

Aidha, amesema takwimu za sensa hiyo zina kila kitu cha kumsaidia mwananchi kukamilisha mipango yake hususani ya kimaendeleo.

Makinda ambaye ni Spika mstaafu alitoa kauli hiyo alipotembelea banda la Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea katika Barabara ya Kilwa, wilayani Temeke.

"Pia kupitia sensa hii, tunaweza kujenga hata utulivu wa kweli ndani ya nchi kwa kuwa mtu hawezi kunung`unika kwa sababu anaona kwamba kila kitu kiko wazi," alisema Makinda.

"Na taarifa zetu zipo za aina mbili, nyingine ni za hesabu ikionyesha idadi ya watu wote nchini, mikoa, wilaya mpaka ngazi ya kitongoji, tunafahamu idadi ya wanawake na wanaume, watoto wenye ulemvu na vitu kama hivyo."

Aidha, alisema endapo wananchi watafahamu umuhimu wa takwimu za sensa wakati wote watakuwa wanazungumza kuhusu maendeleo.

"Na kuna taarifa nyingine ambazo mtu anaweza kuziona kupitia ramani, na anaweza kuona mpaka kijiji anachotaka na vinginevyo," alisema Makinda.

"Na lengo la Rais Samia Suluhu Hassan lilikuwa wananchi washiriki katika sensa hiyo kwa ajili ya maendeleo yao. Ndio maana unakuta kaulimbiu yetu sasa hivi tunasema, matokeo ya sensa ya sita ni mipango jumuishi kwa maendeleo endelevu."

Alisema hakuna bajeti inayoweza kupangwa bila kuwa na takwimu sahihi za kuwesesha hilo.

Alisema kwa mfano mtu akiwa diwani wakati mwingine anajiamulia tu kwamba labda shule ijengwe hapa au pale, wakati mwingine tayari huduma hiyo ipo eneo hilo, kwa hiyo kwa kutumia takwimu za sensa inatusaidia kutuongoza katika mipangilio yetu ya maendeleo au huduma mbalimbali," alisema Makinda.

# Ndege zisizo rubani kudhibiti uvuvi haramu, vyanzo vya maji

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA inatarajia kutumia ndege zisizo na rubani 'drones' katika bahari kuu na vyanzo vingine vya maji, ili kudhibiti uvuvi haramu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba maalum wa kuwa mwenyeji wa mkutano wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS), utakaofanyika Septemba 9 hadi 13, mwaka huu.

Mkataba huo ulisainiwa kati ya Tanzania iliyowakilishwa na Prof. Shemdoe pamoja na OACPS iliyowakilishwa na Katibu Mkuu Msaidizi, Cristelle Pratt.

Wengine walioshuhudia utiaji saini wa mkataba huo ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Edwin Mhede, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Jestas Nyamanga na wajumbe wa kamati ya maandalizi ya mkutano huo kutoka wizarani.

Prof. Shemdoe alisema, pia wanakusudia kutumia teknolojia mbalimbali kudhibiti uvuvi wa mlipuko na njia zingine haramu zinazotishia maisha ya viumbe wa baharini.

"Tunataka kutumia ndege zisizo na rubani kujua nani anafanya nini na wapi, tunataka kutumia teknolojia hiyo katika kudhibiti uvuvi haramu ambayo ni miongoni mwa masuala muhimu yatakayojadiliwa wakati wa mkutano huo," alisema Prof. Mdoe.

Kuhusu mkutano wa OACPS, Prof. Shemdoe alisema utawaleta nchi wanachama 79 ambao ni mawaziri na wataalamu wanaoshughulika na sekta ya uvuvi pamoja na uchumi wa buluu.

Alisema mawaziri hao watatoa maazimio kuhusu sera zitakazotungwa kwa ajili ya uokoaji wakati wa majanga na mambo mengine katika bahari.

Aidha, mkutano huo pia utajadili namna wananchi wanavyoweza kunufaika na Bahari ya Hindi kupitia uchumi wa buluu, sekta ya uvuvi, usafirishaji, kilimo cha mwani, utunzaji wa bahari na kudhibiti uvuvi haramu.

"Kuna mambo kadhaa yatakayojadiliwa katika mkutano huo ikiwamo jinsi watu wanaozunguka vyanzo hivi vya maji wanavyoweza kunufaika na rasilimali zikiwamo za uvuvi, za majini na mengine ikiwamo vita dhidi ya uvuvi haramu," alisema Prof. Shemdoe.

Naye, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Nyamanga alisema mkutano huo ni fursa kwa Tanzania ambayo imeonesha nia ya kuendeleza uchumi wa buluu na kuna fursa mbalimbali kwa wawekezaji ikiwamo uvuvi na kilimo cha mwani.



## Wanahabari wazindua mradi kuhifadhi mazingira

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Wanahabari ya Usaidizi wa Jamii za Pembezoni (MAIPAC), imezindua mradi wa uhifadhi wa mazingira, kwa kutumia maarifa ya asili katika Halmashauri ya Monduli mkoani Arusha.

Mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF), kupitia programu ya miradi midogo ambayo inasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Monduli, Mkoa wa Arusha, Isack Joseph alizindua mradi huo jana katika hafla iliyofanyika Mto wa Mbu, Wilaya ya Monduli.

Alisema halmashauri hiyo ipo tayari kutoa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuhifadhi maarifa ya asili, ambapo watu watakuja kujifunza mila, tamaduni na maisha ya jamii za asili.

Mkurugenzi wa MAIPAC, Mussa Juma, alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu ya pili, ambapo awamu ya kwanza ilikuwa Wilaya ya Longido, Ngorongoro na Monduli na sasa ni wilaya mbili za Karatu na Monduli.

Alisema lengo la mradi huo ni kusaidia uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo kwa maarifa ya asili.

Juma alishukuru GEF, UNDP na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kuendelea kutoa fedha kwa MAIPAC, ili itekeleze miradi ya mazingira na kutunza vyanzo vya maji.

Alisema kwa mara kwanza MAIPAC inakwenda kukusanya maarifa ya asili ya jamii ya wahadzabe na datoga, ili yaweze kuhifadhiwa na kutumika katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Ofisa Wilaya ya Karatu, Reginald Hallu alisema wilaya hiyo kama wilaya nyingine zinakabiliwa na changamoto ya uharibifu na mazingira, hasa kwa wananchi kulima katika vyanzo vya maji.

Hallu alisema halmashauri imekuwa ikichukuwa hatua mbalimbali kudhibiti hilo na kuipongeza MAIPAC kuungana na serikali na kupeleka mradi wa mazingira Ziwa Eyasi.

Ofisa Misitu wa Tarafa ya Manyara, Happy Masaki alisema mwaka juzi MAIPAC ilikuwa na mradi wa mazingira katika kata ya Selela na aliomba wajengewe uzio chanzo cha maji Kabambe na anashukuru MAIPAC kukubali na mwaka huu wanajenga.

Ofisa miradi wa Shirika la Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF) Stevin Ngowi na Mkurugenzi wa Shirika la MPDO, Lebaraka Laizer ambao mashirika yao yanafadhiliwa na UNDP, pia walieleza MAIPAC limekuwa shirika la mfano kwa kutekeleza vyama miradi.

# Wadau watoa neno kuelekea uchaguzi mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa maendeleo nchini, likiwamo Shirika la TUSONGE CDO, wamesihi vyama vya siasa kufuata namna bora ya kuwapata wagombea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la TUSONGE CDO linalofanya kazi zake katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Singida, Aginatha Rutazaa, alisema kuna mambo mengi wao kama wadau wa maendeleo wanayaona yanawarudisha nyuma kina mama kujitokeza kugombea nafasi hizo.

"Tunaloliona hasa ile mifumo ya vyama vya siasa, kuna kuwa na mambo mengi yanayorudisha nyuma kina mama kuingia katika mchakato wa uchaguzi na kuweza kufanikiwa. Moja ile mfumo au taratibu za vyama vya siasa, unakuta kuna vigezo ni kama kwa makusudi vinaondoa Kina mama nje," alisema na kuongeza:

"Watu kama wale wanaoitwa 'wajumbe' waangaliwe upya. Hao ndani ya vyama wakati mwingine hawatendi haki, kwa sababu kuna mgombea mmoja ana maslahi na anajua namna ya kucheza nao ili kupata kura zao na kuwashinda wengine hata kabla ya kura za maoni. Makundi kama ya watu wenye ulemavu unakuta ile mifumo iliyoandaliwa haiangalii kwa upana kiasi hicho".

Aidha, Rutazaa, aliiomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Tume Huru ya Uchaguzi nchini (INEC), kuboresha mahitaji ya jamii ya watu wenye ulemavu katika uchaguzi huo na ule wa mwaka 2025.

Rutazaa alifafanua: "Kuna watu wanaohitaji maandishi ya nukta nundu, kuna watu wanaohitaji labda tafsiri ya mkalimani katika zoezi zima, unakuta havipatikani".

Aliongeza: "Lakini hata miundombinu ambayo inatumika katika kuendeshea zoezi lile, mingi unakuta ni ofisi za serikali ngazi za kata na kwenye ngazi za mitaa, vijiji na unakuta majengo yake ni yale yaliyojengwa siku za nyuma hayafikiki kwa watu wenye ulemavu wanaotumia viti mwendo".

Vilevile alisema: "Tuliiomba serikali hayo yazingatiwe na zoezi lile linajumuisha kila mtu, basi maeneo na ule ujumuishaji wa dhati uangaliwe ili kila mtu aweze kuingia katika mchakato huo."



Mdau wa maendeleo wa wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Taiko Ole Kulunju (wapili kulia) akizungumza na msimamizi wa kituo cha watoto cha Light In Africa, kilichopo mji mdogo wa Mirerani, Mary Moria baada ya kuwatembelea na kutoa msaada wa chakula na fedha iliyogharimu Sh. milioni 1, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Kituo cha afya chaunganishwa umeme wa jua

**Na Gwamaka Alipipi**

KITUO cha Afya Themi jijini Arusha kimeondokana na adha ya kusitisha huduma pindi umeme unapokatika, baada ya kuunganishwa na mfumo wa nishati ya jua.

Kituo hicho kinachohudumia wakazi wa Njiro na maeneo jirani jijini hapa, kimeingizwa kwenye mfumo huo na kampuni ya Sun King inayojihusisha na usambazaji wa nishati ya jua.

Awali, huduma kituoni hapo zilikuwa zikisitishwa pale panapotokea changamoto ya kukatika kwa umeme na kuwa kero kwa wagonjwa, kwamba mtambo huo utawezesha maabara ya kituo hicho kufanya kazi kwa saa 24.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya mtambo huo, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Charles Sululu, alisema msaada huo wa kuunganishwa kwenye mfumo wa umeme wa jua utasaidia sana katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema baada ya kufunga sola hiyo umeme utakatika lakini watapata huduma muda wote, kina mama watahudumiwa, watoto watapata huduma zikiwa nzuri.

Akizungumza baada ya kuzindua ofisi hizo na kukabidhi mradi huo, Meya wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Maxmillian Iranghe, alipongeza kampuni hiyo kwa kusaidia kituo hicho na kuwa itasaidia utoaji bora wa huduma za afya hasa kwa kina mama na watoto.

Alisema mfumo huo wa nishati ya jua utasaidia kuokoa maisha ya wagonjwa kituoni hapo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Kijamii Halmashauri ya Jiji la Arusha, Isaya Doita, alisema mbali na ofisi hiyo kuajiri vijana wengi ila mchango walioutoa kwenye sekta ya afya utasaidia kuboresha sekta hiyo ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi.

Aidha, Makamu wa Rais wa Kampuji hiyo anayeshughulikia mauzo nchi za Afrika, Victor Agandi, alisema wameguswa na juhudi za serikali kufikisha huduma za afya kwa wananchi na wao wameona wachangie.

Alisema moja ya shughuli wanazofanya ni kurudisha sehemu ya faida kwa jamii na kuwa wametoa msaada huo kwa lengo la kuboresha sekta ya afya ili wananchi wapate huduma za uhakika na bora.

## Jeshi la Polisi laja kisasa mapambano ukatili

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi mkoani Manyara, Wilness Kimario, amesema kwa sasa jeshi hilo limekuja na utaratibu mpya wa kuwatumia wapelelezi maalum kila wilaya.

Amesema wapelelezi hao tayari wameandaliwa kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia, ambayo yamekithiri kwa sasa nchini.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), ngazi ya mkoa.

Alisema kwa sasa kila wilaya ina wapelezi maalum wa siri ambao wanafanya kazi kwa siri katika kushughulikia vitendo vya ukatili ambavyo vinaathari kwa kiwango kikubwa kwa watoto na wanawake.

Aidha, alisema bado kuna tatizo la vitendo vya ukatili na masuala ya ukatili yanaanzia katika jamii ambapo wapo wanaume wanawalawiti watoto mpaka wa miaka mitano na wengine kuwabaka.

Kaimu Katibu Tawala wa mkoa huo, Dominick Mbwete, alishauri kila mzazi, mlezi aendelee kuweka mkazo kwenye shughuli ambazo zinalenga kulinda ustawi wa watoto kuanzia ngazi ya chini.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Ibrahim Yeo, alisema miongoni mwa vikwazo wanavyokabiliana navyo ni mila potofu na baadhi ya wazazi kushindwa kuchangia chakula cha mchana shuleni na hivyo kusababisha watoto wengine kuingia kwenye vishawishi.

Meneja mradi wa mtoto kwanza kutoka shirika la COSITA, Agustino Balohho, aliwaomba wataalamu kuwajibika ipasavyo, ili kukomesha vitendo vya ukatili kwa watoto kwasababu bado hali ni mbaya kwa watoto chini ya miaka minane wengi wanabakwa na kulawitiwa.





# RC amfuta 'machozi' bibi anayepigania ardhi kuuzwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi amempatia mawakili wa kumsaidia mkazi wa mkoani Mara, Joyce Matiku (66) katika kesi dhidi ya mtoto wake, Joseph Matiku anayemshtaki kwa kuuza nyumba pamoja na shamba.

Kesi hiyo iliyofika hadi ngazi ya Mahakama Kuu lakini haikuwa inapata maamuzi kutokana na makosa ya ufunguaji kulikosababishwa na kutokuwa na wanasheria wa kumsimamia.

Joyce alifikisha kilio chake mbele ya Mkuu wa Mkoa huyo, katika utaratibu wake wa kusikiliza kero za wananchi ofisini kwake na kutoa maamuzi mbalimbali.

Kanali Evans baada ya kumsikiliza Joyce na kufuatilia vielelezo muhimu, alimpatia mawakili watakaomsaidia kufungua upya kesi hiyo ili itolewe maamuzi sahihi na ya haki kwa mujibu wa sheria.

Aidha, alimueleza Joyce kuendelea kuishi katika nyumba hiyo iliyouzwa mpaka pale maamuzi ya mahakama yatakapotolewa baada ya kuwa amesimamiwa na mawakili aliompatia.

**Kesi hiyo iliyofika hadi ngazi ya Mahakama Kuu lakini haikuwa inapata maamuzi kutokana na makosa ya ufunguaji kulikosababishwa na kutokuwa na wanasheria wa kumsimamia.**

Katika hatua nyingine, Kanali Mtambi amewasilikiza wananchi wa Kijiji cha Bumangi, Wilaya ya Butiama ambao eneo lao walilopanga kujenga soko lilitolewa kwa makosa na dalali wa mahakama katika kesi ya talaka baina ya wanandoa wawili na eneo hilo kupewa mke wa wanandoa hao.

Katika maamuzi yake, Kanali Mtambi aliwataka viongozi hao kuendelea kulitumia eneo lao lililogawiwa katika kesi ya talaka ya wanandoa hao na kama kuna mtu atakuja kuwaondoa wawataarifu viongozi wa Wilaya ya Butiama na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Kadhalika, Kanali Mtambi aliwasikiliza wananchi wanaoidai fidia Manispaa ya Musoma baada ya maeneo yao kutumika kujenga shule za sekondari za kata kufika ofisini kwake wakiwa na vielelezo vyao ambapo pia Mkurugenzi na baadhi ya maofisa kutoka manispaa hiyo wataitwa kujibu hoja zao.



Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko (wa pili kushoto) akimkabidhi kompyuta mpakato Rashid Sikwala, ambaye ni Katibu wa Muloku Amcos kilichopo huko Ilolangulu wilayani Uyui, mkoani Tabora. Wengine ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora Said Mkumba (kulia). **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Machifu watakiwa kuwarithisha mila vijana

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amewaomba machifu kuwarithisha vijana mila na desturi nzuri zenye kulinda maadili katika jamii.

Macha alitoa kauli hiyo juzi kwenye hitimisho la tamasha la utamaduni la kabila la Wasukuma Sanjo ya Busiya, Kijiji cha Negezi Kata ya Ukenyenge wilayani Kishapu kwenye Ikulu ya Chifu Makwaia.

Alisema serikali inatambua matamasha ya utamaduni, ambayo yanadumisha mila na desturi, hivyo kuwaomba machifu kuwarithisha vijana mila hizo zenye tija na kulinda maadili.

Aidha, aliwataka kuweka pembeni na kukemea mila potofu zisizo na tija ili kukilinda kizazi dhidi ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

"Machifu washawishini vijana na kinamama wenyesifa, wajitokeze kugombea nafasi za uongozi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na Uchaguzi Mkuu mwakani ili kutimiza haki yao ya kikatiba," alisema Macha.

Chifu wa kabila la wakamba kutoka Kaunti ya Kitui nchini Kenya Dk. Augustus Muli, alisema wamefurahi kuona utamaduni wa kabila la wasukuma na kwamba matamasha kama hayo yanaunganisha watu kuwa wamoja, huku akipongeza pia kuona vijana wakirithishwa masuala ya mila na desturi za kabila hilo.

Chifu Edward Makwaia wa Sanjo ya Busiya, alisema kila mwaka wanaandaa tamasha hilo la kitamaduni, kuanzia Julai na kuhitimishwa katika Sikukuu ya Saba Saba ambapo pia serikali hutumia fursa ya kusukuma ajenda zake mbalimbali kwa kufikisha ujumbe kwa wananchi.

# Ubovu wa mitumbwi wawaliza wavuvi wa dagaa

**Na Restuta Damian,** KAGERA

BAADHI ya wavuvi wa dagaa kutoka katika mwalo wa Nyamkazi uliopo Kata ya Miembeni Manispaa ya Bukoba wameziomba mamlaka husika kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mitumbwi inayotumika wakati wa shughuli za uvuvi ili kudhibiti ajali majini.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakizungumza na Nipashe na kueleza kuwa ukaguzi huo pia uambatane na kuwahimiza wamiliki kufanya matengenezo ya mara kwa mara, ili kuwaepushia ajali za majini pindi wanapoingia kufanya shughuli za uvuvi.

Mmoja wa wavuvi hao. Kened Atanaz alisema mitumbwi imekuwa ikipasuka pindi wakiwa katika shughuli zao hali inayo walazimu kusimama, huku maji yakiendelea kuingia ndani ya mtumbwi hali inayohatarisha maisha yao.

"Mara kadhaa tumekuwa tukikabiliana na hali hii ambapo maji yanaingia kwa kasi ndani na kusababisha mtumbwi kuanza kuzama wakati huo mtu anakuwa katikati ya maji ya kina kirefu ambako hakuna msaada, hivyo wengi kupotea majini," alisema Atanaz.

**Alisema tayari kazi hiyo imefanyika katika baadhi ya maeneo ambapo walibaini kuwepo kwa mitumbwi chakavu inayohitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa ili ziendele kufanya shughuli zake.**

Mvuvi mwingine, Hemed Ismail alisema jinsi ajali zinavyotokea nchi kavu hata ndani ya ziwa zinatokea kutokana na vyombo kuharibika, hivyo kutaka ukaguzi unaofanyika nchi kavu utiliwe mkazo pia kwenye vyombo hivyo.

Mmiliki wa mitumbwi katika mwalo wa Nyamkazi, Alfredina France alisema kama wamiliki hufanya ukarabati wa vyombo hivyo kulingana na jinsi vinavyoingiza pesa.

"Mategemeo hatuwezi kufanya kabla haijaingiza pesa kwani ni sawa kufanya biashara ya hasara, licha ya kuwepo kwa upepo unaovuma ziwani unakuja na mawimbi na unaleta shida ya kupasua mitumbwi na kuweka uwazi unaokupenyeza maji, hivyo tunajitahidi kurekebisha panapowezekana,"alisema mmiliki huyo.

Ofisa Mfawidhi wa Shirika la Wakala wa Meli nchini (TASAC), Mkoa wa Kagera, Mzee Mvihanga alisema moja ya shughuli zao ndani ya maji ni pamoja na kukagua usalama wa vyombo vya hivyo.

Alisema tayari kazi hiyo imefanyika katika baadhi ya maeneo ambapo walibaini kuwepo kwa mitumbwi chakavu inayohitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa ili ziendele kufanya shughuli zake.

Alisema katika ukaguzi huo vyombo 10 vimesimamishwa ili vifanyiwe ukarabati mkubwa na kurudi majini, ikiwa ni katika maeneo ya Kemondo, Kelebe na Magarini, hivyo kuahidi kufika katika maeneo ambayo bado hawajakagua.



Kinu na mtwangio teknolojia ya karne nyingi zaidi duniani

Ukurasa 14



Ukurasa 13

Unayedaiwa mkopo kampeni ya 'fichua' inaanza na wewe



Ukurasa 14

Zije marathoni kuchangia elimu kuacha vyakula vyenye sumu

Nipashe TESA
Jumanne Julai 9, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

TEKNOLOJIA

NA BEATRICE PHILEMON

# Taka plastiki sasa ni 'baraka' wenye bajaji, magari na boda

KUNA msemo kuwa taka ni fursa tena ni pesa. Hili linadhihirishwa na kile kinachofanywa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), ambayo kwa kurejeleza taka za plastiki, imeibua fursa kibao.

Mosi imewaletea vijana ajira, ambao wanafurahia kuuza plastiki na kujipatia mapato, taasisi inazalisha vipuri kupunguza kuagiza kutoka nje na kubwa zaidi DIT imefanikisha ulinzi na utunzaji wa mazingira, anasema Meneja Uzalishaji, Abdul Lwangisa.

Anaongeza kuwa DIT inarejeleza kwa kuchakata chupa na taka za plastiki kutengeneza vipuri vya magari, pikipiki, bajaji na mitambo mingine.

Anaeleza kuwa ni mafanikio yaliyopatikana baada ya kufanya utafiti na kuona kuwa taka za plastiki zipo nyingi mitaani na pia uhitaji wa vipuri vya mitambo, magari, pikipiki na bajaji ni mkubwa na haujapata majawabu.

Akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Meneja Uzalishaji wa DIT, anasema waliamua kugeuza changamoto ya taka za plastiki kuwa fursa na kuongeza kipato kwa jamii na taifa.

"Wananchi wanaokusanya taka hizi na kuuza wanapata fedha, nasi tunapozalisha vipuri kama rubber boot ambayo ni mipira ya kuzuia tope na maji yasiingie kwenye beringi za tairi.

"Bush rabbers ambayo ni mipira ya kuzuia mikwaruzo ya chuma kwa chuma kwenye vyombo vya moto na corn rubber mipira inayowekwa kwenye matairi ya bajaji kuzuia tope na maji visiingie" anasema."Lwangisa.

Anataja vipuri vingine kuwa ni 'spring bushes, vifaa vinavyowekwa kuzuia msuguano kati ya vyuma na vyuma na vingine ni 'hydraulic oil seal, escalator, elevator roller na chicken plucker' kuwa vyote hupatikana.

Anasema pamoja na kuzalisha vipuri wameanzisha kiwanda cha kuchakata taka za plastiki ndani ya taasisi hiyo iliyoko katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Lwangisa anafafanua kuwa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha vipande 3,500 vya 'corn rubber' kwa ajili ya bajaji, spring bushes za magari 4,500 na vipande 4,000 vya suspension bushes vya pikipiki, vyote vikizalishwa kwa siku moja.

" Kwa wananchi au wafanyabiashara wanaohitaji vipuri hivi vyote vimethibitishwa ubora na Shirika la Viwango (TBS ), bei zetu ni nafuu na bidhaa zinapatikana kwa urahisi,"anasema Lwangisa.



Meneja Uzalishaji, Abdul Lwangisa, akielezea matumizi ya vipuri wanavyotengeneza kwa taka za plastiki. **PICHA: DIT**

### MAKUNDI WANUFAIKA

Meneja Uzalishaji , anasema wanapata taka za plastiki kutoka kwa vijana, wanawake na makundi ya wenye mahitaji maalumu, wakinunua tani mbili za taka kwa siku wakiwafuata wauzaji katika maeneo yao.

"Kilo moja inanunuliwa kwa Sh 300 au 450 kulingana na hali ya soko," anasema Lwangisa

Mbali na hilo, pia teknolojia hiyo ilishindanishwa na vyuo 16 vya elimu vilivyo chini ya Wizara ya Elimu Tanzania Bara na Visiwani, kwenye Mashindano ya Sayansi na Teknolojia Kitaifa yaliyofanyika Dodoma mwaka 2019.

Anasema: "Teknolojia yetu ya kuchakata taka za plastiki ilichukua nafasi ya pili kwa ubunifu bora wa mashine na bidhaa zinazolenga kuwakomboa wananchi kiuchumi na kutunza mazingira."

Lwangisa anasifu juhudi hizo akisema teknolojia hiyo iko sokoni kusaidia wananchi wanaomiliki vyombo vya moto kupata vipuri kwa bei nafuu na pia vinavyodumu na vyenye ubora.

"Tunapatikana Dar es Saalam hapa DIT, kwa Dodoma tupo Majengo, Arusha- Ngarenaro, Songwe tunapatikana mtaa wa kwa Mpemba, wakati tuko Uyole kwa upande wa Mbeya Uyole na Mwanza ni kwenye kampasi ya DIT," anasema Lwangisa.

Anasema vijana 30 wana ajira na wanaendesha maisha yao kutokana na mradi huo.

### KUPATA TEKNOLOJIA

Meneja huyo anasema DIT inafundisha teknolojia hiyo kwa wanafunzi wake ili wakihitimu wafungue kampuni zao,kujiajiri, kuwa wajasiriamali na kuajiri wengine kuongeza kipato na kupunguza uharibifu wa mazingira.

" Wapo wanafunzi watano katika taasisi yetu wanasoma kozi fupi ya kuchakata taka za plastiki na pia wapo wengine kutoka viwandani wanaofika DIT kujifunza,"anasema na kuongeza kuwa taasisi inapokea watu wenye elimu ya darasa la saba hadi ya vyuo vya elimu ya juu.

Mnufaika wa bidhaa hizo Domina Lwakatare kutoka Chanika Dar es Salaam, anapongeza teknolojia hiyo ya kuchakata taka za plastiki kwa sababu zimekuwa ni changamoto kubwa kitaifa.

Anasema watu wanazitupa hovyo zinaharibu mazingira, nyingine zimejaa mtoni, maziwani na baharini wakati wa mvua zinaziba mitaro mitaani na makazi yanakuwa machafu na mazingira kuchafuliwa.

Anasema kwenye maziwa na mito zinaathiri samaki na viumbe wengine na kuharibu mifumo yote ya ikolojia kama wataalamu wanavyosema.

Domina anasema ingawa taasisi hiyo imeanzisha mradi huo ,wananchi waelimishwe jinsi ya kukusanya taka na kuzihifadhi ikibidi DIT wapanue maeneo ya uzalishaji ili wawanufaishe wananchi mikoani.

Aidha, anasema kuelimisha wananchi mbinu na umuhimu wa urejelezaji taka ili kutunza mazingira uwe ajenda ya kudumu kwenye mikutano ya vijiji, mitaa na kwenye nyumba za ibada ili kufanikisha kampeni hiyo.

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kinu na mtwangio teknolojia ya karne nyingi zaidi duniani



Kutwanga kwenye kinu hakuna umri hata watoto wanaweza. **PICHA: MTANDAO**

KAZI ya kuandaa nafaka au vitu vingine vinavyokobolewa, kusagwa na kupondwa ili kupata unga na bidhaa nyingine leo hufanywa kwa kutumia mashine za kisasa.

Ukiingia jikoni zipo mashine, mfano, blenda zikisaga matunda kupata juisi, hutengeneza mtori, hutumiwa kusaga nyanya na kuchanganya vyakula vya watoto. Pia, hata nazi hukunwa kwenye mashine zinazotumia umeme.

Lakini, lazima pembeni kuna kinu kinachotumiwa kuponda kisamvu, kutwanga viungo, karanga, kweme, dawa na wakati mwingine kupwaga nafaka ambazo mashine huenda haziwezi kazi hiyo.

Kinu na mchi ni zana za siku nyingi na inayoendelea kutumiwa na kwa kutazama kazi zake , teknolojia ya kuponda na kusaga vyakula imeboreshwa zaidi.

Kwa Tanzania karne nyingi na karibuni kabla ya Uhuru 1961 matumizi ya mashine kusaga nafaka, kuzikoboa au kupwaga hayakuwepo, karibu nchi nzima kilitumika kinu na mtwangio. Baadhi ya jamii ziliongeza pia jiwe la kusagia ili kuponda au kutwanga nafaka.

Nafaka kama mahindi, mchele, mtama, uwele na ulezi vilipitia mchakato huo, lakini leo kazi hiyo imerahisishwa kwa kutumia mitambo inayoendeshwa kwa umeme, dizeli au petroli kusaga, kukoboa na kushughulikia nafaka hizo.

Kinu ndicho kinachokoboa, kuponda, kupwaga na , kutwanga nafaka kama mahindi, mtama, mchele na uwele ili kujipatia unga uwe wa ugali, chapatti, uji, mikate, vitumbua na nafaka za kupika kande.

Teknolojia hiyo ya kinu cha asili, inatumika hadi leo mijini na vijini mfano huponda kisamvu mijini na vijijini, wapo wanaokoboa mpunga, wengine hukoboa na kutwanga kahawa, kutwanga mlenda, dawa mbalimbali za binadamu na wanyama.

Kinu cha asili ya Tanzania kinatokana na mti gogo linakatwa na kutengeneza shimo katikati kutegemeana na ukubwa unaotakiwa. Vipo vyenye ujazo mdogo, vingine hufikia hata debe au ndoo nzima. Ili kutwanga unahitajika mtwangio ambao ni mti pia.

Kuna upande huwa mpana au mkubwa zaidi na mwingine mwembamba lengo ni kuuwezesha ufae kwenye matumizi mbalimbali kuanzia kuponda a hadi kupwaga hasa mahindi au mtama.

> "Familia zilisaga mbegu kama karanga, korosho, mbegu za maboga, wakati mwingine hata dawa. Kwa ujumla ilikuwa kazi ngumu ndiyo maana kinu kilihitajika.

Kinu kinaweza kuwa na mitwangio mbalimbali hata mitano.

Kinu kinatumiwa kuondoa maganda ya nje ya nafaka hasa mahindi, mtama, mpunga na uwele wakati mwingine maji hutumika kulowanisha hasa mahindi, japo mpunga hayatumiki.

Kinu ni teknolojia inayoendelea kutumiwa hata leo ndiyo maana utakikuta mijini na vijijini. Hakuna jiko lisilokuwa na kinu japo kidogo ili kutwangwa viungo mbalimbali vya pilau na vingine vya kuunga vyakula.

Kinatumika kutwanga mboga mfano mlenda, kisamvu, kadhalika dawa za aina mbalimbali zinazotumiwa mijini na vijijini.

Makabila mbalimbali ya Tanzania yanakitumia kifaa hiki na yamekipa jina , mfano Kipare ni 'kitwi na 'mthi', Wasukuma huita 'litoli na mwisi' wakati Kihaya huitwa 'ekinu na emutwangilo.'

Historia ya kuponda mazao mbalimbali ili kuandaa chakula kwa karibu dunia nzima au jamii zote ziwe maskini au za matajiri ilianza kwa kutwanga ndipo ulikuwa mwanzo wa ujio wa kinu.

Kutwanga au kuponda nafaka ambazo ni chakula muhimu ili kupata nguvu kwa jamii nyingi, kulikuja na ugunduzi wa kinu na mtwangio hasa vya miti, japo kuna madai kuwa vipo vinu vya mawe ya granite hasa huku Asia.

Mchakato wa kuandaa vyakula ulihusisha pia kuwa na jiwe la kusagia, ambalo jamii zilikuwa nalo kuanzia zama za Masiha Yesu Kristo hata na Tanzania na Afrika nzima. Mfano Nigeria kuna jiwe hilo ambako kwa Wayoruba linaitwa olo.

Jiwe hili lilitumika nyumbani kusaga mahindi, mtama, ngano, mihogo kupata unga.

Familia zilisaga mbegu kama karanga, korosho, mbegu za maboga, wakati mwingine hata dawa. Kwa ujumla ilikuwa kazi ngumu ndiyo maana kinu kilihitajika.

Watafiti wa akiolojia na anthropolojia wanaoangalia mienendo ya mambo ya kale wanaeleza kuwa kabla ya wanadamu kuwa na moto jiwe la kusaigia,kinu na mtwangio vilihusika na ndicho kiwanda cha chakula.

Ni chombo cha kwanza cha kutayarisha chakula, kinu kikitajwa kuwa ni cha zamani miaka mingi kabla ya ujio wa Kristo.

Inaelezwa kuwa chombo hicho kilitumika kwa ajili ya masuala ya kiroho kwenye jamii za Wahindi ili kuwaepusha na mapepo na magonjwa.

Lakini pia kinaweza kuonekana kuwa kifaa hicho kina historia ya kutumiwa China, Misri na nchi nyingine za Afrika.

Kadhalika akiolojia inaonyesha jinsi kilivyotumiwa kuandaa nafaka za kupikwa kwenye sherehe za kidini za Warumi na hata Waamerika wa asili maarufu Red Indians.

Kuna ukweli kuwa kote duniani kwenye watu wa utamaduni mbalimbali walikuwa na jiwe la kusaga nafaka na baadaye kikafuata kinu na mtwangio kuandaa vyakula vyanafaka.

Kwa baadhi ya jamii kinu kilitumiwa vibaya kilikuwa kitanzi cha watoto waliokuwa hawatakiwa na jamii mfano wenye ulemavu, kwa mfano Wapare kabla ya Uhuru na ujio wa mafundisho ya dini, wanadaiwa walijaza maji kwenye kinu na kuwatumbukiza watoto hao kichwa chini miguu juu ili kuwaua.

**UMUHIMU**

Ni kifaa kinachotumika maeneo mengi muhimu karibu dunia nzima. Kikiwa na sura tofauti hata leo kinatumika maabara za utafiti, jikoni, kwenye viwanda vya dawa na hata wanaotoa tiba za asili.

Kwa upande wa uchongaji kinu na mtwangio ni urembo huchongwa na wana sanaa za kuchonga vinyago, wapo wanaotumia 'marble' , soapstone,' na mpingo lakini pia udongo wa mfinyanzi kuviunda.

Kwa ujumla kinu na mtwangio ni teknolojia inayoendelea kuishi na huenda itachukua karne nyingi kuondoka.

ELIMU
NA DK.REUBENI LUMBAGALA

# Unayedaiwa mkopo kampeni ya ‘fichua’ inaanza na wewe

ELIMU ni nyenzo ya kumwezesha mtu kumudu na kutawala mazingira ambayo ndiyo maisha yake. Ni wazi unapopata maarifa, stadi na ujuzi ni msaada wa kujua namna ya kuendesha maisha kwa kuwa yale uliyojifunza unayatumia kusongambele.

Kimsingi, elimu ni ghali, ni gharama, ndiyo maana kuendesha na kutoa elimu, serikali, asasi za kiraia, mashirika, mataifa washirika wa maendeleo na wananchi wamekuwa bega kwa bega kuchangia maendeleo ya elimu.

Wanatoa fedha, kugharamia mafunzo ya walimu, sare, kujenga miundombinu, vifaa vya ujenzi, na vya wanafunzi, kompyuta, samani na vifaa vya michezo ili kuwezesha elimu kuwafikia wanafunzi popote katika mazingira bora yanayochochea uelewa.

Serikali mdau namba moja wa kila kitu anawapa mikopo wanafunzi wa vyuo vya kati na vikuu ili kumudu gharama za elimu ya juu kuanzia kujikimu, ada, chakula, malazi, vitabu na mafunzo kwa vitendo .

Ili kuratibu kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo, ipo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), iliyoundwa tangu 2004, ikihusika na kupokea maombi, kuyachakata na mwisho kutoa orodha ta waliokidhi vigezo vya kupata mikopo.

Kwa wale waliokidhi kupata mikopo, wanapata taarifa za kiwango au asilimia za mikopo walizopata ili kujua gharama nyingine wanazopaswa kuchangia na kuzisaka kabla ya kuingia vyuoni.

Mathalani, mwanafunzi aliyepata mkopo wa asilimia 80 na ada ya kozi yake ya chuo kikuu ni Shilingi 1,000,000 kwa mwaka, bodi ya mikopo itampatia mnufaika Sh.800,000 naye ataongezea 200,000 kukamilisha ada kwa mwaka.

Ikumbukwe kuwa HESLB haitoi msaada wa fedha bali inakopesha wanafunzi kwa mkataba kuwa atakapohitimu, arejeshe mkopo uliotumika kumsomesha ili pesa hizo zitumike kusomesha wengine sasa na miaka ijayo.

Kwahiyo, kila mnufaika wa mkopo, anapaswa kuurejesha baada ya kuhitimu akiajiriwa au kujiajiri.

Kwa walioajiriwa katika sekta binafsi au ya umma wanapaswa kurejesha asilimia 15 ya mshahara wao wa kila mwezi na kwa




Wahitimu wanapofurahia mahafali wakumbuke kurejesha mikopo ya bodi. **PICHA: MTANDAO**

wale waliojiajiri wanayo fursa ya kuwasiliana na HESLB na kuweka utaratibu wa kiwango cha fedha wanachoweza kurejesha kila mwezi kulingana na vipato.

Ili kuongeza wigo wa marejesho ya fedha kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, HESLB imekuja na kampeni “fichua kuwa hero wa madogo” ili kuwamulika na kuwafichua wanufaika walio na ajira lakini hawarejeshi fedha zilizowasomesha.

Kampeni hii maalum ya kuwasaka wadaiwa sugu 50,000 ili kukusanya Sh.bilioni 200.

Fichua inayozinduliwa rasmi Juni 28, 2024 na itaendeshwa kwa miezi miwili ikilenga kuongeza makusanyo ya mikopo kw kuwafichua wanufaika ambao licha ya kuwa na ajira haleti rejesho HESLB.

Mkurugenzi wa HESLB Dk. Bill Kiwia, akizindua Fichua anasema:“Kampeni hii inalenga kuwashirikisha wananchi kutimiza jukumu la kizalendo la kuwafichua wadaiwa wenye kipato lakini hawajitokezi kurejesha mikopo.”

Wanufaika wawe wazalendo kwa kutambua kuwa fedha zilizotumika kuwasomesha ni za Watanzania ambao walikubali wapewe ili wasome.

Lakini pia ni rejesho la mikopo hiyo kutoka kwa waliowatangulia zilizokusanywa zikapatikana nao wana wajibu wa kuzirudisha

Hivyo basi, wajue wana deni warejeshe fedha hizo hata kama bado hawajaanza kukatwa moja kwa moja kupitia mishahara au ajira binafsi.

Dk. Kiwia anawataka wananchi kuwafichua wadaiwa sugu wa mikopo ili kuwezesha wanufaika wengi zaidi kunufaika na mikopo ya elimu ya juu.

“Ili kutoa taarifa za wadaiwa, mwananchi anapaswa kutuma jina la mnufaika, chuo alichosoma, eneo analofanyia kazi iwe kampuni, kiwanda au asasi, shule kama amejiajiri au kuajiriwa na eneo ilipo taasisi hiyo,” anasisitiza Dk. Kiwia.

Wananchi waiunge mkono HESLB kwa kuwafichua wadaiwa sugu ili kuongeza makusanyo ili Watanzania wengi zaidi wapate fursa ya kufikia elimu ya juu.

**JIFICHUE MWENYEWE**

Pamoja na kwamba HESLB imeanzisha kampeni hiyo, ni vyema mnufaika yeye mwenyewe akajifichua kwa kuwasiliana na bodi moja kwa moja ili kuweka utaratibu wa kulipa mkopo wake kupitia namba maalum ya malipo (control number) hasa waliojiajiri wenyewe.

Kujifichua ni uzalendo kwa kuzingatia kuwa waombaji wengi wa mikopo wanatoka familia maskini ambazo haziwezi kumudu gharama za chuo, kwahiyo kujitokeza ni kutambua umuhimu wa kuwezesha wengine kusoma hasa wanaotoka familia maskini.

> “Muhimu zaidi ni kwa wanufaika wenyewe kujifichua kabla ya kufichuliwa wakumbuke kulipa mkopo si mpaka uwe umeajiriwa serikalini au katika sekta binafsi.

**WAAJIRI WAFICHUENI**

Waajiri ni wadau muhimu katika kurejesha mikopo wanufaika hao wanapopata kazi katika ofisi zao. Kwa upande wa waajiri wa serikali, imekuwa rahisi kuwapata kutokana na mifumo iliyopo sasa na ndiyo maana mwajiriwa mpya wa sekta ya umma anapoanza kazi kama alipata mkopo, anaanza kulipa deni kupitia mshahara wake wa kwanza au wa pili anapoanza kazi.

Changamoto ipo kwa baadhi ya waajiri wa sekta binafsi ambao baadhi yao wamekuwa wakificha au kuchelewa kutuma taarifa za wafanyakazi wao ambao baadhi yao ni wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Kwahiyo, kupitia kampeni ya fichua, waajiri wote wa sekta binafsi na umma watoe taarifa sahihi za waajiriwa wao ili serikali kupitia HESLB iweze kukusanya fedha zaidi ili vijana wengi wagharamiwe elimu ya juu.

Muhimu zaidi ni kwa wanufaika wenyewe kujifichua kabla ya kufichuliwa wakumbuke kulipa mkopo si mpaka uwe umeajiriwa serikalini au katika sekta binafsi.

Unaweza kuanza kulipa kidogo kidogo hata kupitia ajira binafsi uliyonayo, mathalani, kwenye kilimo, ufugaji, bodaboda, mamalishe, fundi simu, ususi na ujenzi.

Ikumbukwe kuwa kampeni ya Fichua ni maalum kwa wanufaika ambao wameshahitimu masomo yao na wana kazi za kuwaingizia kipato lakini bado hawajaanza kulipa mikopo hiyo. “Lengo ni kufichua wadaiwa sugu ambao wana vipato, lakini wako mitaani wanaendelea na shughuli zao na hawashtuki kulipa madeni.,” anakumbusha Dk. Kiwia.

***Mwandishi ni mwalimu Sekondari ya Mlali iliyoko Dodoma. M***

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU

# Zije marathoni kuchangia elimu kuacha vyakula vyenye sumu

TANGU mwaka huu umeanza zimekuwepo marathoni kibao na bado zinaandaliwa, kuhimiza kufanya mazoezi ili kujiepusha na maradhi yasiyoambukiza hasa saratani, sukari, figo na shinikizo la juu la damu.

Magonjwa hayo yanaelezwa kuwa chanzo chake ni ulaji na maisha ya kubweteka, yasiyopenda kufanyakazi za kutoka jasho.

Mitindo ya maisha au namna nzima ya kuendesha maisha inatajwa kuwa kisababishi kikuu Watanzania kuwa na maradhi hayo, wakidaiwa kula zaidi nafaka zilizokobolewa kama mchele, ngano na sembe bila kuongeza protini, mboga, matunda na maji ya kutosha kwenye mlo.

Zaidi, mlo wanaotumia unaandaliwa kwa mafuta mengi , ukisindikizwa na vinywaji vinavyozalishwa viwandani vyenye sukari kwa wingi na baada ya kula hukimbilia kitandani au kwenye kochi kupumzika.

Aina hiyo ya ulaji hujaza tumbo na kuongeza vitambi au viriba tumbo, huleta unene kupindukia na wakati mwingine huumiza moyo, figo, mishipa ya fahamu na mifupa. Pia, wataalamu wa afya wanaelezwa kuwa watu wengi hawafanyikazi wala mazoezi, wanazoea kupumzika zaidi, kutumia pikipiki na magari.

Hata hivyo, Watanzania hawajasikia kikamilifu kuhusu kampeni za kupinga kemikali za sumu kwenye vyakula na jinsi tafiti zilivyofanyika hapa nchini na kuibua hatari hizo.

Kula kemikali kwenye vyakula hakuzungumzwi kikamilifu na kupigiwa kampeni, kama zinavyofanyika marathoni za kupunguza uzito kwa kufanya mazoezi.

Kuna haja ya kuanzisha marathoni za kupinga matumizi ya mbolea za viwanda zenye kamikali za sumu kwenye kilimo ikibidi kila mkoa na wilaya ili kupata chakula kisichochafuliwa kuanzia mazao ya muda mfupi hadi mrefu, mayai, nyama na maziwa lengo likiwa kulinda afya ya mlaji na mazingira.

Kampeni za kusisitiza matumizi ya dawa za asilia na zilizo hai (biological) ili kunyunyizia mboga na matunda ya muda mfupi kama matikiti na matango na pia kuhifadhi mazao ili kulinda afya za walaji na mazingira zipewe nguvu zaidi.

Ni wakati wa kutumia marathoni hizo kuhamasisha kutengeneza dawa hai za asili kwa ajili ya kudhibi wadudu waharibifu wa mazao ili kupata mabadiliko ya kiafya na kupunguza maradhi yasiyoambukiza.

Tanzania imejaa miti dawa mingi ambayo inafaa kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao shambani na yaliyovuna.

Kuna mimea kama ndulele, mwarobaini, mapapai dume, pilipili kichaa, aloivera pamoja na majivu ya kuni vyote hivyo ni tiba mujarabu kwa mazao badala ya kemikali za sumu.

Dawa hizo zinafukuza wadudu waharibifu hata kuwaua lakini haina athari kwa mimea na wadudu wengine ardhini na angani, hivyo ni kitu bora kuliko viuatilifu vyenye kemikali za sumu.

Kwa ujumla kutumia dawa za asili hakuna madhara kwa binadamu na hupunguza magonjwa yasiyoambukiza yatokanayo na kemikali mwilini.

Aidha, zinarutubisha udongo na makapi yanayopatikana wakati wa kutengeneza dawa za asili mbolea bora kama ilivyo samadi ya ng'ombe, na kuzuia.

Marathoni za kulinda afya ziwakumbuke wakulima pia, fedha zipatikane wapewe mafunzo na utaalamu waache kutumia dawa za viwandani, wageukie viuatilifu asili na pia lianzishwe soko rasmi la viuatilifu asili kwa sababu ni tiba ya binadamu, wadudu, wanyama udongo, mimea na hazina madhara wala maradhi

Mathalani, mbolea ya chumvi inamiminwa kwenye mchicha wa siku 21, inakaa kwa siku saba,wakati ilitakiwa ukae ardhini hata kwa mwezi mmoja ni wazi kuwa watu wanapotumia pengine hawabaki salama.

Kuna hatari kuwa sumu zinazoliwa zinasababisha athari kwa binadamu hasa maradhi yasiyoambukiza hasa saratani, mishipa ya fahamu na vivimbe mwilini, shida ya ini na figo.

Ikumbukwe mazao yanahitaji virutubisho vya naitrojen (N), fosiforasi (P) na potasiamu (K), ambavyo ni muhimu na vinaleta ukuaji bora, mazao mengi na tija lakini uwepo wa kemikali ni hofu ndani ya viritubisho hivyo vya viwanda, si jambo jema zama hizi.

Virutubisho hivyo vinatokana na mbolea za chumvi chumvi ambazo zina sumu na kemikali zinapoliwa kwa wingi matokeo ni maradhi yasoambukiza pia, hilo tusilisahau tukakimbilia mazoezi huku vyakula vimejaa sumu.

Baadhi ya watalaamu wanazihusisha na kusababisha kuzaliwa watoto wenye mtindio wa ubongo au mama kujifungua kabla ya muda wa miezi tisa, saratani, shida kwenye maini na ngozi

Ni wazi kuwa dawa za viwandani zina athari kubwa hivyo ni wakati wa kuhamasisha marathoni za kila mara ili kupata chakula salama kuanzia kupanda hadi kuhifadhi.

Dawa au viutilifu asili hudhibiti wadudu au visumbufu katika mazao ya mahindi, karanga, mboga, matunda kama papai, tango na matikiti, pamoja na kuhifadhi nafaka kavu.



Mboga zikitibiwa kwa viuatilifu vya viwandani. **PICHA: MTANDAO**

> “Kuna mimea kama ndulele, mwarobaini, mapapai dume, pilipili kichaa, aloivera pamoja na majivu ya kuni vyote hivyo ni tiba mujarabu kwa mazao badala ya kemikali za sumu.

### VIUATILIFU HAI

Vipo viuatilifu hai vingi mfano vya kuua katapila au funza kwenye mazao hadi vya kuhifadhi vyakula ghalani.

Wakulima wanashauriwa kutumia busta asili ambavyo si ngumu kuandaa, mfano ipo ya mbolea mbichi ya ng'ombe, mkulima aweke kilo 20 ndani ya kiroba, akifunge na kukitumbukiza ndani ya pipa la lita 200 isizame ndani bali ifunikwe na maji ikiwa inaning'inia katikati ya tangi hilo.

Mkulima aendelee kupigapiga kila siku na kukoroga maji ndani ya pipa kwa siku 21 au mwezi, baada ya hapo achuje maji kwa kiroba, anayachuja tena kwa kitambaa safi na kuanza kunyunyuzia juu ya majani ndiyo 'busta' hai.

Mbolea hiyo ya majani ina virutubisho vingi na hufanya mmea kukua kwa kasi na kwa tija zaidi.

Kwa upande mwingine mkulima anaweza kutumia majani ya papai dume, kwa sababu hili halizai, akate majani yake na kuyatwanga kwa kipimo kutegemeana na ukubwa wa shamba.

Anaweza kutwanga kilo nne akazichanganya na majivu ya kuni siyo ya mkaa vijiko vinne vikubwa akaloweka kwa siku 10 hadi 14 kwenye dumu la lita 20 ili ichache.

Akiitoa aichuje na kiroba baadaye kitambaa kupata dawa, anayonyunyuzia kwenye mazao wakati makapi yake ni mbolea.

Dawa lazima inyunyuziwe katikati ya mmea mfano mahindi na chini ya majani na siyo juu kwa sababu wadudu huishi chini ya jani kujikinga na jua na maadui.

Pia dawa inyunyuziwe jioni kuanzia saa 10 hadi usiku kutegemeana na upatikanaji wa mwanga na kufanya hivyo kwa kurudiarudia ili kudhibiti visumbufu.

Papai lina kemikali inayoitwa 'papain' yenye sumu ya kuua mdudu kadhalika majivu nayo yana kemikali inayosababisha mdudu kushindwa kupumua.

Mwarobaini pia unatumika, unakaushwa ndani siyo juani, unatwanga na unachanganya na sabuni ya unga, kwa mfano kilo moja ya unga wa mwarobaini unawekwa kwenye lita 10 za maji. Unakorogwa ili kuleta mchanganyiko na kuongeza kijiko kimoja cha sabuni ya unga halafu unafunikwa kwa saa 24.

Baada ya hapo, unachuja mara mbili kwa mfuko wa kiroba mara ya tatu unachujwa kwa kitambaa laini na inakuwa tayari kwenda kunyunyizia shambani.



## Bosi TAMISEMI akoshwa ujenzi barabara za TARURA

**Na Renatha Msungu** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI anayeshughulikia miundombinu, Rogatus Mativila amesema ameridhishwa na ujenzi wa miradi ya barabara za lami zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Alisema hayo baada ya kumaliza ziara yake ya kikazi ya kukagua uimara wa barabara zinazosimamiwa na TARURA ambapo alitembelea miradi minane.

Mativila alisema barabara zote hizo zimejengwa kwa fedha za tozo na mfuko wa maendeleo wa barabara ambazo hutolewa na serikali kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara hususani maeneo ya mijini.

"Nimefurahishwa na viwango vya barabara hizi ambazo zinasimamiwa na TARURA pamoja na makandarasi waliojenga barabara mkoani Dodoma, wamefanya kazi nzuri na hata kwa kuangalia kwa macho barabara zote zipo kwenye viwango vizuri hata wakazi wanaoishi jirani na barabara hizi unaona wanavyofurahia," alisema.

Alisema anaishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara hususani barabara za mijini.

"Sisi tunashukuru sana kwa kutupa maisha bora kupitia miundombinu ambayo Rais Samia aliamua kuongeza fedha na kuhakikisha zinajengwa barabara kwa kiwango cha lami" alisema Mativila.

Akiwa kwenye barababa inayounganisha Dodoma kwenda Singida (Nala) inayoelekea kiwanda cha mbolea cha Itracom Fertilizer Limited (km 5) alisema kwenye sera ya viwanda zipo fedha ambazo serikali imeongeza tozo ambazo zinatumika katika maendeleo ya miundombinu inayoenda kwenye viwanda.

Alisema viwanda hivyo vinatoa ajira kwa Watanzania pia kwa mbolea inayotengenezwa hapo inauzwa kwa bei nafuu.

"Barabara hii inasaidia kiuchumi na kijamii kwani maeneo jirani na kiwanda hiki yamepimwa, hivyo inawarahisishia usafiri pia wakazi wa Dodoma wanapata ajira kupitia kiwanda hiki". alisema.

Mativila alisema barabara hiyo inayoruhusu magari ya kubeba mizigo yenye uzito mkubwa, hivyo kurahisisha usafirishaji wa malighafi kutoka nje ya kiwanda na pia mbolea toka kiwandani na kuwafikia wananchi kwa ajili ya kilimo.

Msimamizi wa miradi wa Barabara ya Swaswa-Mpamaa (Km 8.7), Atuletile Ngailo alisema mradi huo umekuza Uchumi wa wakazi hao pia umewapunguzia umbali kwa kutumia barabara hiyo.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Dodoma, Emmanuel Mfinanga alisema barabara zilizojengwa mjini hapo zimekuwa mkombozi kwa wananchi, kwamba maeneo mengi hayakuwa na barabara hivyo alishukuru serikali kwa kuendelea kupeleka fedha za kutengeneza na kuboresha barabara wilayani Dodoma.

# Wanaotetea, kulinda haki za walimu waanza kuvurugana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAGOMBEA nafasi ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu katika Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA), wamepinga matokeo ya uchaguzi uliofanyika Juni 26, mwaka huu jijini Tanga.

Wagombea hao wamekata rufaa katika Kamati Tendaji Taifa ya chama hicho na kudai kuwa endapo haki haitatendeka watakwenda mahakamani na wengine kudai kurudi Chama Cha Walimu Tanzania (CWT).

Akizungumza na waandishi wa habari, aliyekuwa mgombea nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Nyavidunda Mhule, alisema wamefikia hatua hiyo kutokana na kutoridhishwa na mwenendo wa matokeo ya uchaguzi huo.

Alisema moja kati ya sababu ambazo zimewafanya kupinga matokeo hayo ni mchakato wa uchaguzi kutokuwa halali kutokana na uchaguzi kusimamiwa na mwenyekiti wa muda badala ya kamati ya uchaguzi kwa mujibu wa katiba ya chama hicho Kifungu cha 7 (ix).

"Mchakato wa uchaguzi ulikuwa batili kutokana na matokeo ya uchaguzi kutangazwa na Kamishna wa Kazi badala ya msimamizi wa uchaguzi mmoja kati ya wasimamizi wa uchaguzi watatu waliokuwepo kama katiba ya chama inavyoelekeza"alisema

Alisema dosari nyingine katika uchaguzi huo ni mgombea na mshindi wa nafasi ya mweka hazina hakuwa mwanachama hai kutokana na kutolipa ada ya wanachama kwa miezi sita mfululizo kama katiba inavyoelekeza.

"Lakini uchaguzi pia hakuwa huru, halali na wa haki kutokana na wagombea kutopewa muda wa kujieleza na kunadi sera zao" alisema.

Kadhalika, alisema uchaguzi huo hakuwa huru, halali na wa haki kutokana na kugubikwa kwa vitisho kwa wagombea ambapo ndani ya ukumbi kulijaa askari polisi kinyume na taratibu za uchaguzi.

Aliyekuwa mgombea nafasi ya Katibu Mkuu Taifa, Tumaini Nyagawa, alisema aanapinga matokeo ya uchaguzi huo na kumuomba Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi nchini kuufuta uchaguzi huo.

"Tayari tumeshakata rufaa katika Kamati Tendaji Taifa tunasubiri majibu kama hakutakuwa na majibu ya kuturidhisha basi tutakwenda mahakamani kupiga matokeo ya uchaguzi" alisema Nyagawa.

Mmoja wa wanachama hicho, Hilary Mwingira alisema kutokana na ubabaishaji wa chama hicho ambao umeanza kuonekana mapema aliwashauri walimu wenzake kurudi CWT.




Msanifu Majengo na Mshauri Elekezi kutoka Chuo cha Ufundi Arusha, Richard Idelya, akitoa maelezo kuhusu ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Singida kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka huu ,Godfrey Mnzava (wa pili kutoka kushoto). Wa kwanza kutoka kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kiongozi wa mwenge atoa maagizo dawa za mbu

**Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

HALMASHAURI za wilaya nchini zimeagizwa kuweka utaratibu wa kununua dawa ya kupuliza kwa ajili ya kuua mazalia ya mbu katika robo ya kwanza au ya pili ya kila mwaka wa fedha, lengo likiwa ni kutokomeza ugonjwa wa malaria.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mnzava, alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida.

"Kuna mtindo kwenye halmashauri suala hili linapelekwa mwishoni kabisa kwenye mwaka wa fedha. Unasikia hii tunatekelezaga robo ya mwisho, sikatai labda kutokana na jiografia lakini kwanini dawa ikinunuliwa robo ya kwanza au ya pili je ita-expire? mbona dawa nyingine zinanunuliwa," alihoji.

Alitoa agizo hilo baada kuelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023 dawa hizo hazijapulizwa katika halmashauri hiyo.

Mnzava alisema suala siyo la bajeti ambapo zinahitajika Sh. milioni moja kununua dawa wakati uwezo wa halmashuri kukusanya mapato yake ya ndani ni zaidi ya Sh.bilioni moja.

Mratibu wa malaria katika Halmashauri ya Itigi, Monica Paul, alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2023 vyandarua 56,678 vilitolewa kwa wazee na wajawazito na watoto waliopata chanjo ya surua walikuwa 11,573.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imetenga Sh.milioni 1.492 katika kipindi cha mwaka 2023/2024 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na upuliziaji wa viuwadudu ambazo Sh.600,000 zimeshalipwa kwa ajili ya kununua lita 46.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, alisema atahakikisha anasimamia suala la ununuzi wa dawa katika halmashuri ili kutimiza lengo la serikali la kutokomeza ugonjwa wa malaria.

TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MBEYA REGION
## 00783037 - CHUNYA DISTRICT COUNCIL

# FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2023

| | Note | 2023 TZS | Restated 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 2,096,991,941 | 494,523,730 |
| Receivables | 67 | 257,687,092 | 249,886,626 |
| Prepayments | 69 | 68,130,546 | 475,905,164 |
| Inventories | 70 | 371,109,567 | 365,654,448 |
| Other Financial Assets | 71 | 99,735,750 | 96,283,000 |
| Total Current Asset | | **2,893,654,896** | **1,682,252,968** |
| Non Current Asset | | | |
| Investment Property | 76 | 508,800,000 | 511,320,000 |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 35,034,045,166 | 28,581,264,480 |
| Work In Progress | 82 | 4,003,008,473 | 4,233,357,168 |
| Total Non Current Asset | | **39,545,853,639** | **33,325,941,648** |
| TOTAL ASSETS | | **42,439,508,535** | **35,008,194,616** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current Liabilities** | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 702,770,839 | 2,092,805,926 |
| Deferred Income | 93 | 1,090,391,329 | 124,144,239 |
| Deposits | 94 | 392,351,007 | 92,781,220 |
| Total Current Liabilities | | **2,185,513,175** | **2,309,731,385** |
| Non Current Liabilities | | | |
| Other Borrowings by Government Entities | 102 | 75,951,057 | 120,738,110 |
| **Total Non Current Liabilities** | | **75,951,057** | **120,738,110** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **2,261,464,232** | **2,430,469,495** |
| **Net Assets** | | **40,178,044,302** | **32,577,725,121** |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| Capital Contributed by: | | | |
| Other Reserves | | 76,553,000 | 76,553,000 |
| Accumulated Surpluses / Deficits | | 40,101,491,302 | 32,501,172,121 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | **40,178,044,302** | **32,577,725,121** |

Signature:...............
Name: Hon. Bosco Mwanginde
Council Chairperson
Date: 29.9.2024

Signature:...............
Name:- Tamimu Kambona
Council Director
Date: 29.9.2024

## CASHFLOW STATEMENT AS AT 30th JUNE, 2023

| | NOTES | 2023 TZS | Restated 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | |
| **RECEIPTS** | | | |
| Subvention from other Government entities | 32 | 25,099,984,925 | 23,151,736,940 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 1,369,597,495 | 907,780,879 |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 122,929,022 | 284,433,285 |
| Other Revenue | 31 | 1,029,292,965 | 647,631,555 |
| Levies | 18 | 2,769,691,834 | 2,182,247,953 |
| Increase in Deposit | 61 | 299,569,787 | 0 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 706,817,142 | 1,369,727,239 |
| **Total Receipts** | | **31,397,883,170** | **28,543,557,851** |
| **PAYMENTS** | | | |
| Wages,Salaries and Employee Benefits | 34 | 17,358,907,595 | 13,189,198,098 |
| Use of Goods and Service | 35 | 4,821,859,268 | 5,172,517,618 |
| Social Benefits | 43 | 437,175,200 | 1,324,551,966 |
| Other Transfers | 60 | 447,817,946 | 364,205,320 |
| Other Expenses | 52 | 46,270,205 | 363,213,164 |
| Maintenance Expenses | 36 | 114,715,480 | 2,716,516,570 |
| Decrease in Deposit | 61 | 0 | 54,249,219 |
| **Total Payments** | | **23,259,240,908** | **23,184,451,955** |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | 8,171,137,476 | 5,359,105,895 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | | |
| **Investing Activities** | | | |
| Payment for Work in Progress | 106 | -3,063,630,973 | -2,656,678,464 |
| Advance Payment for Acquisition of Property Plant and Equipment | 103 | -68,130,546 | -475,905,164 |
| Acquisition of Property,Plant and Equipment | 77 | -3,392,120,694 | -2,729,619,153 |
| **Total Investing Activities** | | **-6,523,882,213** | **-5,862,202,781** |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | **-6,523,882,213** | **-5,862,202,781** |
| **CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | | |
| **Financing Activities** | | | |
| Cash repayments of amounts borrowed | 97 | -44,787,053 | -17,135,924 |
| Cash proceeds from other short or long-term borrowings | | 0 | 4,016,063 |
| **Total Financing Activities** | | **-44,787,053** | **-13,119,861** |
| **NET CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | **-44,787,053** | **-13,119,861** |
| **Net Increase** | | 1,602,468,211 | -516,216,746 |
| Cash Surrendered to Holding Account | | 0 | 0 |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | | 494,523,730 | 1,010,740,476 |
| Cash and cash equivalent at end of period | | 2,096,991,941 | 494,523,730 |

Signature:...............
Name: Hon. Bosco Mwanginde
Council Chairperson
Date: 29.9.2024

Signature:...............
Name:- Tamimu Kambona
Council Director
Date: 29.9.2024

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE AS AT 30TH JUNE, 2023

| | Note | 2023 TZS | Restated 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| **Revenue** | | | |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 147,164,022 | 298,123,285 |
| Levies | 18 | 2,693,782,340 | 2,056,475,193 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 706,817,142 | 1,369,727,239 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 1,369,597,495 | 907,780,879 |
| Fair value Gains on Assets and Liabilities | 24 | 3,452,750 | 5,179,125 |
| Other Revenue | 31 | 1,029,292,965 | 645,066,446 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 25,032,130,335 | 24,330,714,529 |
| **Total Revenue** | | **30,982,237,049** | **29,613,066,696** |
| **TOTAL REVENUE** | | **30,982,237,049** | **29,613,066,696** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Wages,Salaries and Employee Benefits | 34 | 16,014,959,527 | 13,260,321,696 |
| Use of Goods and Service | 35 | 5,540,484,606 | 6,296,967,295 |
| Maintenance Expenses | 36 | 114,715,480 | 2,716,516,570 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 37 | 795,057,340 | 476,256,331 |
| Depreciation of Investment Property - Carried at Cost | 38 | 2,520,000 | 2,520,000 |
| Loss on Disposal of Assets | 44 | 0 | 69,377,211 |
| Other Expenses | 52 | 46,270,205 | 350,087,755 |
| Social Benefits | 56 | 437,175,200 | 1,324,551,966 |
| **Total Expenses** | | **22,951,182,358** | **24,496,598,824** |
| **Transfer** | | | |
| Other Transfers | 60 | 430,735,510 | 394,400,000 |
| **Total Transfer** | | **430,735,510** | **394,400,000** |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **23,381,917,868** | **24,890,998,824** |
| Surplus / Deficit | | 7,600,319,181 | 4,722,067,871 |

Signature:...............
Name: Hon. Bosco Mwanginde
Council Chairperson
Date: 29.9.2024

Signature:...............
Name:- Tamimu Kambona
Council Director
Date: 29.9.2024

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Unqualified Opinion**

I have audited the financial statements of Chunya District Council which comprise the statement of financial position as at 30 June 2023, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Chunya District Council as at 30 June 2023, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the section below entitled "Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements". I am independent of Chunya District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key Audit Matters**

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

### 1.2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

#### 1.2.1 Compliance with the Public Procurement Laws

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performed a compliance audit on the procurement of works, goods and services of Chunya District Council for the financial year 2022/23 as per the Public Procurement Laws.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, procurement of goods, works and services of Chunya District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Laws.

**(i) Use of micro procurement method for transactions above the threshold of 5 million - TZS 53,559,340**

I noted payments of TZS 53,559,340 were made to various staff for procuring items for Uhuru torch activities, construction of football playground and other Council activities but exceeded the limit set out in the Seventh Schedule of Regulation 166 (4) of the PPR, 2013 that requires a procuring entity to use petty cash, imprest or purchase cards to effect payments under micro procurement which is not above TZS 5,0000,000.

**(ii) Inappropriate procurement method used for acquisition of goods - TZS 288,362,810**

I noted that, Chunya District Council procured goods worth TZS 288,362,810 using competitive quotations (shopping) instead of the National competitive tendering method contrary to Regulation 149 (1) of the PPR, 2013 and Seventh Schedule that set national competitive tendering be applied for goods cost above TZS 120,000,000.

#### 1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines

**Subject matter: Budget formulation and execution**

I performed a compliance audit on budget formulation and execution of Chunya District Council for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, Budget formulation and execution of Chunya District Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**March 2024**



## HABARI ZANZIBAR

# Mawaziri EAC wajadili utatuzi migogoro ya kisiasa, usalama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamekutana Zanzibar kujadiliana namna ya kutatua migogoro ya kiusalama na kisiasa inayozikumba nchi zao, kuja na azimio moja.

Naibu Waziri Mkuu wa Uganda, Rebecca Kadaga na Waziri Kiongozi katika Baraza la Mawaziri Kenya, Musalia Mudavadi ni miongoni mwa washiriki wa mkutano huo ambao ni utekelezaji wa agizo lililotolewa na marais wa nchi.

Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walitoa agizo kwa mawaziri hao wakutane kwa faragha kutafuta namna bora wa kuimarisha amani, usalama na kuharakisha muungano wa kisiasa baada ya mafanikio kuanza kuonekana katika forodha na ushuru wa kibiashara.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Veronica Mueni Nduva, alisema mkutano huo umejumuisha mataifa yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema wanataka uhusiano wa mambo ya usalama, biashara yanaimarishwa kwa sababu Afrika wanafanya biashara zaidi nje, hivyo lazima kuwepo kwa miundombinu ambayo itarahisisha kufanya biashara ikiwemo miundombinu ya barabara, mawasiliano na masuala ya kifedha bila ya vikwazo.

**Naibu Waziri Mkuu wa Uganda, Rebecca Kadaga na Waziri Kiongozi katika Baraza la Mawaziri Kenya, Musalia Mudavadi ni miongoni mwa washiriki wa mkutano huo ambao ni utekelezaji wa agizo lililotolewa na marais wa nchi.**

"Lazima kuwa na mikakati na mipangilio wa masuala ya usalama kwa sababu usalama ukikosekana kwa taifa moja hatimae utafika kwa jirani" alisema.

Wakitoa salamu zao wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, mawaziri kutoka Burundi, Uganda, DRC, Somalia, na Kenya walisema kuwa amani, usalama na muungano wa kisiasa ni mambo yanayohitaji kuwekewa mikakati ili kufikia mafanikio.

Waziri wa Mambo ya Nje Kenya, Musalia Mudavadi, alisema kuwa Zanzibar ni sehemu nzuri ambayo yenye utulivu wa kupata muda wa kujadiliana mambo mbalimbali na kupata ufumbuzi sahihi baada ya kuwasilisha matokeo ya mkutano huo.

Alisema watapata fursa ya kujadiliana masuala ya amani, umoja, biashara ili jumuiya hiyo iendelee kuwa na manufaa kwa wananchi wanaounganisha jumuiya hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba alisema mkutano huo utawapa nafasi kuzungumza kinagaubaga na kwa uwazi zaidi changamoto zilizopo katika jumuiya hiyo na kufanyiwa kazi.

Alisema pia wanajadili kwa kina mahusiano ya nchi na nchi katika nchi wanachama ambapo katika kujadili mambo hayo yanahitaji utulivu.

## Wanahabari watakiwa kufuata sheria, miongozo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Ame Khamis amevitaka vyombo vya habari kufuata sheria na miongozo iliyowekwa na tume katika kuandaa na kuripoti habari kwa jamii.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa mafunzo kwa wadau wa habari kuhusu wajibu wa kuzingatia maudhui ya utangazaji na mwongozo wa kuripoti habari katika kipindi cha uchaguzi, yaliyofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar.

"Vyombo vya habari ndiyo tunavyovitegemea katika kuleta maendeleo ya nchi, hivyo basi nina imani kubwa mafunzo haya yatakuwa chachu ya kufanya mabadiliko chanya katika jamii na kudumisha amani ambayo ndiyo imetawala katika nchi yetu hasa katika kipindi tunachoenda cha uchaguzi" alisema.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdullah Salim, alivitaka vyombo vya utangazaji kusajiliwa na kupatiwa leseni, ili kufanya kazi zake kihalali akisema kutofanya hivyo ni kufanya makosa na kwenda kinyume na sheria zilizowekwa.

Mrajis wa Tume ya Utangazaji, Mohammed Said Mohammed alisema vyombo vya habari wanaporusha maudhui wanapaswa kuzingatia staha na maudhui yanayoendana na mila na silka ya jamii.

Mrajis wa Idara Habari Maelezo, Jamila Mahmoud Juma aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha kabla ya waandishi wao kufanya kazi wahakikishe wamepatiwa vibali kutoka Idara ya Habari Maelezo.

**Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdullah Salim, alivitaka vyombo vya utangazaji kusajiliwa na kupatiwa leseni**




Baadhi ya viongozi wa vikundi na mashirika yasiyo ya kiserikali wakiwa katika mkutano wa kujifunza jinsi ya kutoa maoni kuhusu Dira ya Taifa ya mwaka 2025 hadi 2050, ulioandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Viongozi wa dini watakiwa kuhamasisha mshikamano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid amewataka viongozi wa dini kuhamasisha mshikamano utakaodumisha amani na utulivu nchini.

Alitoa wito huo katika maadhimisho ya mwaka mpya wa kiislamu 1446 baada ya kushiriki katika maandamano yaliyoanzia Maisara Unguja, huku viongozi wa dini wakiomba mwaka mpya uwe na baraka katika kuimarisha amani na utulivu.

Zuberi alisema amani ndiyo itakayowawezesha viongozi waliopo madarakani kutekeleza mipango ya maendeleo iliyopangwa katika bajeti za serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2024-2025.

Alisema katika mwaka wa fedha wa bajeti Serikali ya Zanzibar imejipanga kutekeleza na kusimamia miradi ya kimkakati ya kuleta maendeleo ambayo utekelezaji wa mafanikio yake ni kuwepo kwa amani.

"Zanzibar tunasherehekea mwaka mpya wa kiislamu 1446 hijria ambapo wananchi tunahitaji mshikamano mkubwa na kuwaombea viongozi wetu wa kitaifa kupata nguvu ya kutekeleza malengo yao ambapo yote yatafanikiwa kama kutakuwa na amani na utulivu wa kudumu" alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman alisema uamuzi wa kusherehekea mwaka mpya ni wa busara, kwamba unatoa nafasi kwa Wazanzibari kujitafakari katika utekelezaji wa shughuli zao mbalinbali ikiwemo za kuleta maendeleo pamoja na ibada.

"Mwaka mpya wa kiislamu ni fursa adhimu kwa waislamu kujitafakari na kujua malengo yetu tunakwenda wapi katika mustakabali mzima wa kufanya ibada"alisema.

Mjumbe wa Baraza la Maulamaa, Sheikh Zulfikal aliipongeza serikali kwa kuchukua uamuzi wa kuufanya mwaka mpya wa kislamu kuwa siku ya mapumziko, kwamba itakuwa ikisherehekewa kitaifa tofauti na miaka ya nyuma.

Aidha, Shekhe Hassan Ali Muombwa ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Fatwa katika Ofisi ya Mufti alisema mwaka mpya wa kiislamu ni fursa ambayo itaiwezesha jamii hiyo kujikumbusha mambo mengi yenye mnasaba katika kumcha Mungu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMILIANA DONALD LUOGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA NYARAKA ZA VYETI VYAKE, CHETI CHA KUZALIWA KILICHOTOLEWA NA SHIRIKA LA USAJILI WA UFILISI NA UAMINITIA[RITA], CHETI CHA FORM FOUR CHENYE INDEX NAMBA **S0534-0029** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA ST.ANTONY SECONDARY SCHOOL,CHETI CHA FORM SIX CHENYE INDEX NAMBA **S0692-0534** KILICHOTOLEWA NA BARAA LA MITIHANI KUPITIA ROZMIN SECONDARY SCHOOL,CHETI CHA CHUO KIKUU KILICHOTOLEWA NA CHUO KIKUU CHA ARDHI TANZANIA. KWA YEYOTE ATAKAEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/133664/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CATHERINE MARIE- LOUISE WILHELMINE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota RAV 4** yenye namba za usajili **T128ARQ,** Chasis namba **SXA110183166** na Engine namba **3S-2464648.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MAN/MBU/06874/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**PIENSIA FOCUS NGURUWE** anatangaza kupotea pikipiki aina ya **BOXER** zenye namba za usajili **MC 800 DMR , MC 375 DQB ,MC 156 DSF BOXER** na **MC272 CBT SANLG..** Kwa yeyote atakaeziona atoe tarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/136886/2024 NA PHQ/PWA/MKU/12839/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ISRAEL MBUNJU MLOWE** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya **FEKON** na **BOXER** zenye usajili namba **MC 919 BEC**, **MC 305 BQK, MC 269 BUP, MC 251 CQK.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/137415/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AYUBU RAPHAEL MKAGILA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA RUMION** yenye usajili namba **T 522 EGJ na** CHASSIS NAMBA **NZE1511048705.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote chab polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/RUV/SON/3417/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUDI HASHIM MGIMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3579/0043** kilichotolewa na baraza la taifa kupitia **EBENEZER SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/133993/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MUHEZA**

**YAH: MAOMBI NA.29 YA MWAKA 2024**

**WALLACE VINCENT MUNGA.............................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**TITUS JAMES YOHANA ...................MJIBU MAOMBI NA. 1**

**HAZILINA MSENGA ZAKARIA..........MJIBU MAOMBI NA.2**

**WITO**

**HAZILINA MSENGA ZAKARIA** popote ulipo, unafahamishwa kuwa **WALLACE VICENT MUNGA** amefungua shauri ( Maombi) mbele ya Baraza la ardhi na nyumba wilaya ya Muheza dhidi yako lenye na. 29/2024 shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 24/07/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo basi unatakiwa kufika siku hiyo. Vielelezo vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya baraza la ardhi na Nyumba (W) Muheza. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na maamuzi kutolewa dhidi yenu.

Ofisi za Baraza zipo wazi katika Ofisi ya Mtendaji kata kwemkabala. AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri/lakiri ya Baraza hili leo tarehe 05/06/2024

MHINA E. R.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 92 YA 2024**

**SCOVIA JEREMIA KAMUGUNYA................MTETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **EDWARD MUSELETA NYAKIROTO**
2. **NOLIC CAMPANY LIMITED**
3. **TANZANIA COMMERCIAL BANK**
4. **LONGIDO AUCTION MART........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**NOLIC CAMPANY LIMITED**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na nyumba Wilaya Morogoro tarehe 11/07/2024 mbele ya Mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maomba yatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolea uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza leo tarahe 02 mwezi july,2024.

M. KHASIM
MWENYEKITI.

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 297 YA MWAKA 2023**

**RODRICK W. MAGAWA..............................................MDAI**

**VERSUS**

**YOHANA METANE. KAMOGO............................MDAIWA 1**

**GODFREY JOHN JOACHIM...............................MDAIWA 2**

**KWA:**
**GODFREY JOHN JOACHIM**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWAKUWA;** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
**KWAHIYO;** unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 12.08.2024 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08 ya Mwezi wa SABA, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 14958 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BILSON KIZURI MBEZIBWA DECEASED OF MLIMWA C, DODOMA REGION**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOACHIM KIZURI MBEZIBWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 05 day of 08 ...................... 2024
Dated at Dodoma this 02 Day of 07................2024

MAGISTRATE ............ RESIDENT MAGISTRATE DODOMA

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEHEMIA M JAMES,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index No **S0601/0102** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Serengeti Day Mwaka 2017. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/28300/2024**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**ARUSHA SUB REGISTRY**
**(LABOUR DIVISION)**
**AT ARUSHA**

**REVISION NO 37 OF 2023**
**Case Reference: 20237010000508786**
**(Originating: CMA/ARS/ARS/227/22/115/22)**

**NOTICE OF MENTION**

**SALIM MOHAMED MANONGA...........APPELLANT**
**VERSUS**
**JAMBO FOOD PRODUCT LIMITED...........RESPONDENT**

**TO: SALIM MOHAMED MANONGA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mentionin the high court at Arusha on the **10th Day of July 2024** at 9:00 o'clock in the forenoon, before **Hon. D.D. Ndumbaro, Judge.**

You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of you appearance on that day and time before Mention or hearing the court may proceed in your absence.

**GIVEN under my HAND** and the **SEAL** of the **COURT** this 04th day of July, 2024

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT
ARUSHA

**Summons to appear ( O.V, P.20 (1) OF (CPC)**
**(Substituted service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**MISC LAND APPLICATION NO.14709 OF 2024**

**NAIMA ABDUL PESSA AND ANOTHER......APPLICANTS**

**VERSUS**

**TAALUMA WOMEN GROUP & OTHERS......RESPONDENTS**

**TO: ROBERT ODUNGA**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS :** The above named **APPLICANT** has instituted the **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or advocate or authorized agent on 29th day of July, 2024 at 11:00 AM for MENTION before **Hon. S. MWAIPOPO – Judge** to answer the said appeal and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply in support of your reply.
**TAKE NOTICE** that , in default of your appearance on that day, the said matter will be heard and determined in your absence .
Given under my hand and the seal of this court, this 05th day of July, 2024

DEPUTY REGISTRAR


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Umoja wa Mataifa wabaini Rwanda ina vikosi DRC

**NEWYORK,** Marekani

RIPOTI ya wataalam wa Umoja wa Mataifa imesema wanajeshi 3,000 hadi 4,000 wa Rwanda wanapigana pamoja na waasi wa M23 nchini Jamhuri ya Kidomekrasia ya Congo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ambayo imeonekana na shirika la habari la AFP, Kigali inaongoza harakati za waasi hao wa M23.

Mkoa wa Kivu Kaskazini umekuwa ukishuhudia uasi wa wapiganaji wa M23 tangu mwishoni mwa mwaka wa 2011, na kufanikiwa kuchukua baadhi ya miji kwenye eneo hilo.

Serikali ya DRC inaituhumu Rwanda kwa kuwaunga mkono na kuwafadhili waasi hao, madai ambayo yamepingwa.

Licha ya Rwanda kukana madai ya kuwasaidia M23, Ripoti iliyozinduliwa na baraza la usalama la Umoja wa Mataifa limeeleza kwamba hatua ya nchi hiyo kuwaunga mkono waasi hao ina maana kwamba inawajibikia vitendo vinavyotekelezwa na wanamgambo hao.

Ripoti hiyo aidha ilieleza kwamba wanajeshi wa Rwanda (RDF) kupitia oparesheni zao katika maeneo ya Nyiragongo, Rutshuru na Masisi katika jimbo la Kivu Kaskazini ziliwasaidia wapiganaji wa M23 kuchukua maeneo zaidi kati ya mwezi Januari hadi mwezi Machi mwaka huu.

Wataalam hao vilevile walisema kwamba wakati wakiandika ripoti hiyo Mwezi Aprili, idadi ya wanajeshi wa Rwanda ilikuwa inatosha au kuzidi ile ya waasi wa M23.

Ripoti hiyo ina picha, video zilizonaswa na ndege zisizo na rubani, rekodi za video, ushuhuda na intelenjisia inayothibitisha matukio ya wanajeshi wa Rwanda kuvuka mpaka.

Video na picha pia zinawaonyesha watu wenye silaha wakiwa na mavazi rasmi wakiwa na magari ya kivita, vifaa vya kuzuia makombora sawa na malori ya kuwabeba wanajeshi.

Aidha ripoti hiyo pia iliongeza kuwa kuna watoto kuanzia miaka 12 wamesajiliwa kutika kambi zote za wakimbizi nchini Rwanda ambao wanatarajiwa kupelekwa katika kambi za mafunzo katika maeneo yanayokaliwa na waasi chini ya uongozi wa wanajeshi wa Rwanda na waasi wa M23.



Waasi wa M23

# Mrengo wa kushoto washinda Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

MUUNGANO wa vyama vya mrengo wa kushoto nchini Ufaransa umepata ushindi wa kushangaza baada ya miezi michache ya kuundwa kwake.

Kulingana na uchaguzi ulioitishwa mapema, muungano huo umeshinda viti vingi zaidi katika duru ya pili, huku chama chenye msimamo mkali wa kizalendo, National Rally kikiambulia nafasi ya tatu.

Muungano huo unaoitwa New Popular Front (NFP) ulipata ushindi wa kushtukiza dhidi ya chama cha mrengo wa kulia cha National Rally katika duru ya pili ya uchaguzi wa bunge.

Hata hivyo, hakuna muungano umeweza kupata wingi wa kujitosheleza kuunda serikali kivyake.

Ukosefu wa wingi viti kwa vyama hivyo unatishia kuitumbukiza Ufaransa katika msukosuko wa kisiasa na kiuchumi.

Matokeo ya mwisho yatatolewa kati ya Jumapili jioni au Jumatatu.

Uchaguzi huo uliitishwa wiki nne tu katika kile ambacho wadadisi walikitaja kama kucheza kamari kwa Rais Emmanuel Macron.

Chama cha NR, kinachoongozwa na Marine Le Pen kimeongeza idadi ya viti vyake, lakini kimeshindwa kufikia matarajio yake.

Kiongozi wa muungano wa NFP, Jean-Luc Melenchon, alisema wako tayari kuunda serikali na kumuomba Rais Macron, kuwaalika rasmi.

Jana wafuasi wa muungano wa mrengo wa kushoto walikusanyika katika uwanja wa Stalingrad jijini Paris, kufuatilia matokeo na kila mara walionekana kushangilia kwa kupiga makofi wakati chati ikionekana wakiongoza.

Muungano huo unatazamiwa kuwa na viti 172 hadi 215, huku muungano wa Rais wa Emmanuel Macron wa Ensemble kikitarajiwa kupata nafasi ya pili kwa wabunge 150 hadi 180 na NR cha Marine Le Pen, kikiwa cha tatu kwa kufikisha wabunge 120 hadi 152.

Hata hivyo wachambuzi wa kisiasa wanasema bunge lisilo na chama chenye wingi wa wazi linaweza kuzitumbukiza siasa za Ufaransa katika machafuko kwa wiki kadhaa za mashauriano kuamua nani atashika nafasi ya waziri mkuu. Kibaya zaidi Rais Macron anaweza kulazimika kuongoza nchi sambamba na waziri mkuu anaepinga sehemu kubwa ya sera zake za mrengo wa kati. **DW**



Mwenyekiti wa Jumuiya ya kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi, Bola Tinubu ambaye pia ni Rais wa Nigeria akiongoza mkutano wa viongozi wakuu wa nchi wanachama juzi. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Senegal kuwabembeleza wanaokimbia ECOWAS

**ABUJA,** Nigeria

JUMUIYA ya Kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), imemtaka rais wa Senegal, Basirou Diomaye Faye, kufanya mazungumzo na nchi za Mali, Niger na Burkina Faso, kufuatia uamuzi wao wa kujiondoa uanachama.

Katika taarifa iliyotolewa baada ya mkutano wa viongozi wa nchi wanachama uliofanyika nchini Nigeria, juzi ilimteua Rais Faye kama mjumbe wake kukutana na viongozi wa nchi hizo tatu ambazo ziliunda muungano wao tofauti baada ya uhusiano na jumuiya hiyo kuwa mbaya kutokana na mapinduzi ya kijeshi.

Wakati wa mkutano huo, Rais wa Tume ya ECOWAS Omar Alieu Touray, alisema kuwa rais huyo wa Senegal ambaye ni kiongozi mdogo zaidi barani Afrika ana sifa zote zinazohitajika kusimamia mazungumzo hayo.

Siku moja kabla ya mkutano huo, viongozi wa kijeshi wa Mali, Niger na Burkina Faso, zilithibitisha kujiondoa katika Jumuiya hiyo katika mkutano wao wa kilele uliofanyika mjini Niamey nchini Niger.

Wakati huo huo, wanajeshi wa Marekani wamekamilisha mchakato wa kuondoka katika kambi yao nchini Niger kabla ya muda wa mwisho wa Septemba 15.

Katika taarifa, nchi hizo mbili zilisema kuwa wizara ya ulinzi ya Niger na Idara ya Ulinzi ya Marekani zimetangaza kukamilika kuondoka kwa wanajeshi wa Marekani na vifaa kutoka kambi 101 huko katika mji mkuu wa Niamey.

Ndege ya mwisho iliyobeba wanajeshi wa Marekani ilitarajiwa kuondoka Niamey jana jioni.

Wizara ya Ulinzi ya Ujerumani pia ilisema itakamilisha operesheni zake katika kambi yake nchini Niger kufikia Agosti 31 kufuatia kuvunjika kwa mazungumzo na viongozi wa kijeshi. **DW**

HABARI MICHEZO

# SINGIDA, COASTAL, JKU, KUFUNGUA KAGAME LEO

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

MICHUANO ya Kombe la Klabu Afrika Mashariki na Kati, inaanza kutimua vumbi leo nchini, wakati timu tatu wenyeji, Singida Black Stars, Coastal Union na JKU zitakapokata utepe kwenye viwanja vya KMC na Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumzia mashindano hayo jana, rais Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ambaye pia ni rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema ni faraja Tanzania kuwa mwenyeji baada ya kutofanyika muda mrefu.

"Timu ambazo zimethibitisha kushiriki zitapata uzoefu kutoka kwa timu watakazokutana nazo pamoja na kuwasaidia wachezaji wetu kujitangaza kupitia mashindano hayo," alisema Karia.

**Katika michuano hiyo, timu zitakazoshiriki ni JKU (Zanzibar), Dekeda FC (Somalia), Coastal Union na Singida Black Stars (Tanzania Bara), Al Wadi FC, Al Hilal na El Merreikh (Sudan), SC Villa (Uganda), APR (Rwanda), Gormahia (Kenya), Banitui (Sudan Kusini), Red Arrows (Zambia) na Djibouti Telkom FC (Djibouti).**

Michuano hiyo ambayo imepewa jina la Dar Port Kagame Cup, inayozishirikisha klabu za Ukanda wa CECAFA, inafanyika baada ya miaka mitatu kupita, ambapo ilifanyika nchini na Express ya Uganda ambao mwaka huu hawatashiriki, ilitwaa ubingwa kwa kuifunga Nyasa Big Bullets bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa Agosti 14, 2021, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

JKU itafungua dimba saa saba mchana itakapocheza dhidi ya Hay Al Wadi ya Sudan, kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, katika mchezo wa Kundi A, kabla ya saa 10:00 jioni, kundi hilo litakuwa na mchezo mwingine ambapo wawakilishi wengine wa Tanzania, Coastal Union kushuka dimbani kwenye uwanja huo huo kupambana na Dekedaha FC ya Somalia.

Mechi za Kundi B, pia zitapigwa leo, ambapo saa 12:00 jioni, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, SC Villa ya Uganda itakipiga dhidi ya El Merriekh Bentiu ya Sudan Kusini, na saa 3:00 usiku, Singida Black Stars ambao ni wawakilishi wengine wa Tanzania wataingia dimbani kupepetana na APR ya Rwanda.

Mechi za Kundi C, zitachezwa kesho, zote zikipigwa kuanzia saa 12:00 jioni, Al Hilal ya Sudan itakipiga dhidi ya Ali Sabieh ya Djibouti, wakati saa 3:00 usiku, Gor Mahia ya Kenya itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Red Arrows kutoka Zambia.

Washindi wawili wa kila kundi watakwenda hatua ya robo fainali, ambapo timu mbili zitakazofanya vema 'best looser', zitaunganishwa na sita zilizopatikana kupata timu nane zitakazocheza hatua hiyo itakayochezwa kwa mtindo wa mtoano.

Bingwa wa michuano hiyo mbali kukabidhiwa kombe pamoja na medali, pia ataondoka na Dola za Marekani 30,000, itakayoshika nafasi ya pili dola 20,000 na ya tatu dola 10,000.

NGOMA...



Kikundi cha ngoma cha Nguruka kikiburudisha katika Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Utalii lililofanyika katika Uwanja wa CCM Bariadi mkoani Simiyu juzi, katika kuenzi Utamaduni wa Wasukuma Kanda ya Ziwa (Lake Zone Cultural and Tourism Festival), lililoandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro one Travel And Tours. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbaraka atua Coastal Union

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imefanikiwa kumsajili straika wa zamani wa Simba, Mbaraka Yusuph (pichani chini), kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao ambacho kinajiandaa na michuano ya Kombe la Dar Port Kagame inayotarajiwa kuanza leo hapa nchini pamoja na mashindano mengine.

Ofisa Habari wa Coastal, Abbas El Sabri, juzi alisema Mbaraka amejiunga na kikosi hicho akitokea Kagera Sugar.

"Tumefanikiwa kuipata saini ya straika huyu, kusema kweli ametusumbua sana, sasa yupo mikononi mwetu, ni rafiki wa nyavu na msumbufu kwa mabeki pia," alisema Sabri.

Mbaraka ambaye ni zao la kikosi cha vijana cha Simba, alipandishwa timu ya wakubwa 2015, lakini mwaka mmoja baadaye alitimkia Kagera Sugar ambako alikipiga hadi 2017, akajiunga na Azam FC.

Straika huyo alijiunga na Namungo 2019 hadi 2020 ambapo alirejea tena Kagera Sugar.

Mbali na straika huyo, klabu hiyo imefanikiwa kupata pia saini ya winga Abdallah Hassan Abdallah, kutoka Bandari ya Kenya.

Mchezaji huyo mwenye uwezo wa kucheza winga zote mbili ni raia wa Kenya.

Kabla ya kutangaza wachezaji hao, Coastal Union ilimtangaza beki wa kati raia wa Uganda, Anguti Luis, kutoka KCCA ya Uganda.

"Tunaendelea na usajili, lengo ni kufanya vema katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la Shirikisho barani Afrika na hata Kagame ambalo tutaingia kama washindani halisi na si wasindikizaji," alisema Sabri.




# *KMC FC yashusha straika kutoka Cameroon*

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonekana haitaki masihara kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu, Klabu ya KMC imemsajili straika, Ajoh Austin, kutoka Klabu ya Union Sportive ya Cameroon.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, juzi alisema wamemsajili mshambuliaji huyo kwa mkataba wa miaka miwili na lengo kubwa ni kutibu tatizo sugu la ushambuliaji katika kikosi hicho ambalo lilionekana msimu uliopita.

"Niko hapa kuwathibitishia wana Kinondoni na wapenda soka nchini kote kuwa tumefanikiwa kukamilisha uhamisho wa mshambuliaji wa Kimataifa wa Cameroon, Ajoh kutoka Klabu ya Union Sportive.

Ni straika mwenye kasi, nguvu na uwezo mzuri wa kufunga mabao, amekuja kutuongezea nguvu kuelekea msimu ujao kufikia malengo ya klabu na kuwapa furaha wana Kinondoni," alisema Ofisa Habari huyo.

Ajoh anakuwa ni mchezaji wa sita kusajiliwa na kikosi hicho kilichomaliza nafasi ya tano msimu uliopita.

Tayari KMC imeshawatangaza wachezaji, Oscar Paul, kiungo mshambuliaji Mtanzania aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Kenya katika Klabu ya Kakamega Home Boys, beki wa kati, Nickson Kassam Mosha, anayechezea Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 20, akitokea kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar, kipa raia wa Burundi aliyekuwa akiidakia Klabu ya Vipers ya Uganda, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana kutoka, Vital'O ya Burundi na beki wa kati Salum Athumani 'Stopper' kutoka KVZ ya Zanzibar.

## ZISIKUPITE

### CHIESA AWANIWA JUVE

KLABU ya Juventus inataka kumuuza fowadi wa Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26, ili kupata fedha za kumnunua winga wa Manchester United, Jadon Sancho, huku miamba hiyo ya Italia ikifanya mazungumzo kuhusu aina ya ofa ya kumpa mchezaji huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 24. ***(Calciomercato)***

### PALHINHA SAFI MUNICH

KIUNGO wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, amekamilisha matibabu yake na Bayern Munich kabla ya kukamilisha uhamisho wake wa euro milioni 46. ***(Sky Sports in Germany)***

### GARCIA NA LEVERKUSEN

KIUNGO wa kati wa Hispania, Aleix Garcia mwenye umri wa miaka 27, amesema West Ham ilijaribu kumsajili kutoka Girona, lakini alichagua kujiunga na Bayer Leverkusen badala yake. ***(Diari de Girona, via Standard)***

### LLORENTE KUTUA BETIS

REAL Betis imefikia makubaliano na Leeds United kumsajili beki wa Hispania, llorente Diego mwenye umri wa miaka 30, kutoka klabu hiyo ya Elland Road. ***(Marca)***

### KUMRUDIA BRANTHWAITE

MANCHESTER United itafanya mkutano kuhusu uhamisho wa wachezaji ambao utajumuisha uamuzi kuhusu iwapo watatoa ofa nyingine kwa Everton kumsajili mchezaji mwenye umri wa miaka 22 na beki wa kati wa England, Jarrad Branthwaite. ***(Mail)***

### GREENWOOD, MUSTAKABALI

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Mason Greenwood anataka mustakabali wake utatuliwe wiki ijayo, huku Atletico Madrid, Barcelona, Juventus, Lazio, Marseille na Valencia - ambao wamewasilisha ombi la pauni milioni 25, wakimtaka mchezaji huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### BENTLEY AWANIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal inajipanga kumnunua mlinda mlango wa Wolves mwenye umri wa miaka 30, Dan Bentley. ***(Express & Star)***

### GORDON AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City ina nia ya kutaka kumnunua winga wa Newcastle United na England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 23, ambaye mkataba wake unamalizika Juni 2026. ***(Football Insider)***

### CANCELO APEWA OFA

MLINZI wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 30, amepewa ofa kwa Inter Milan na Juventus baada ya kurejea Manchester City kufuatia kukamilika kwa muda wake wa mkopo Barcelona. ***(La Stampa, Via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DESCHAMPS AMTETEA MBAPPE KIWANGO EURO

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amemtetea nahodha wake na mchezaji nyota, Kylian Mbappe, baada ya kukosolewa kutokana na uchezaji wa mshambuliaji huyo katika michuano ya Euro 2024.

**Mbappe mwenye umri wa miaka 25, amefunga mara moja pekee katika michuano hiyo - penalti katika mchezo wa mwisho wa kundi dhidi ya Poland - huku Ufaransa ikifuzu nusu fainali.**

Deschamps alimbadilisha mchezaji huyo aliyesajiliwa hivi karibuni na Real Madrid katika muda wa nyongeza kwenye ushindi wao wa robo fainali dhidi ya Ureno kwa mikwaju ya penalti, huku Mbappe akisema aliomba kutolewa nje.

**Wakati wa maandalizi alikuwa na tatizo kidogo la mgongo, lakini anataka...**

Akizungumza kwenye kipindi cha Televisheni cha Ufaransa cha Telefoot Jumapili, Deschamps aliwakumbusha wale wanaomkosoa Mbappe kile ambacho tayari amepata katika mchezo huo.

"Je, hufikirii kuwa tayari ameweka historia ya kutosha, kwa kile alichokifanya hadi sasa?" alisema kocha huyo.

"Anataka kutengeneza historia zaidi. "Tulifanya kila tuliloweza pamoja naye, pamoja na wafanyakazi wa matibabu, ili kumfanya awe hapa. Wakati wa maandalizi, alikuwa na tatizo kidogo la mgongo, lakini Kylian yuko hapa."

Deschamps pia alijibu mapendekezo kwamba ikiwa hayuko fiti kabisa, Mbappe anaweza kuwekwa benchi ili kujaribu kuanzisha mashambulizi ya timu hiyo. Fowadi huyo amelazimika kucheza sehemu kubwa ya michuano hiyo akiwa amevalia 'maski' baada ya kuvunjika pua kutokana na kugongana na Kevin Danso katika mchezo wa ufunguzi wa kundi la timu yake dhidi ya Austria.

"Hata kama si asilimia 100, najua vizuri kuwa kwa mpinzani, kujua anacheza kunawafanya wafikirie na kuwalazimisha kuzoea," alisema Deschamps.

Ufaransa itacheza na Hispania katika nusu fainali ya Euro leo, Jumanne mjini Munich.

# ZIRKZEE AKARIBIA KUTUA MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inakaribia kukamilisha dili la kumsajili mshambuliaji wa Bologna, Joshua Zirkzee, kwa mujibu wa ESPN.

United imefikia makubaliano mapana juu ya malipo yanayohusiana na wawakilishi wa Zirkzee, ambayo yalikuwa kikwazo na sasa watatafuta kufikia makubaliano na Bologna.

Zirkzee ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 34 katika mkataba wake ambao utatumika hadi Agosti, lakini United wanaweza kutafuta mazungumzo tofauti. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye pia amekuwa akiwiwa na AC Milan, yuko kwenye kikosi cha Uholanzi kinachojiandaa kwa nusu fainali ya Euro 2024 dhidi ya England mjini Dortmund kesho ,Jumatano.

Zirkzee ameibuka kama mshambuliaji anayependekezwa na United baada ya kuwafikiria pia Jonathan David wa Lille na Ivan Toney wa Brentford.

Chelsea pia wameonesha nia ya kumnunua David, ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Lille na anapatikana kwa takriban euro milioni 25. Zirkzee aliifungia Bologna mabao 12 msimu uliopita walipomaliza katika nafasi ya tano kwenye Serie A, na kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza katika enzi ya kisasa.

Chanzo kimoja kiliambia ESPN kwamba United bado inawasiliana na Bayern Munich kuhusu mpango wa kumnunua mchezaji mwenza wa Kimataifa wa Zirkzee, Matthijs de Ligt.

Wajerumani wako tayari kufanya mazungumzo ya kuondoka kwa beki huyo na kumthaminisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kwa zaidi ya pauni milioni 40.



# Araujo aongeza pigo Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imeendelea kukumbwa na majeruhi wiki chache kabla ya kuanza msimu mpya.

Hii ni baada ya mlinzi wa klabu hiyo, Ronald Araujo, kuumia akiwa anaitumikia timu yake ya Taifa ya Uruguay katika michuano ya Copa America.

Araujo alipata majeraha akiwa na Uruguay katika mchezo wa robo fainali dhidi ya Brazil ambapo aliondoka uwanjani akiugulia kwa maumivu makali.

Taarifa zinaeleza kwamba mlinzi huyo atakuwa nje ya dimba kwa muda wa wiki 6 hadi 8.

Hii ina maana kwamba Araujo ataikosa michezo ya mwanzo wa msimu mpya wa 2024-25, kitu ambacho ni pigo kwa kocha, Hansi Flick.

Barcelona pia imepata pigo kutokana na jeraha jipya alilolipata mchezaji Pedri katika huduma yake kwa timu ya Hispania kwenye michuano ya Euro.

# Bayern Munich yamtwaa Olise

**MUNICH,** Ujerumani

MICHAEL Olise amejiunga na Bayern Munich kutoka Crystal Palace, klabu zote zimetangaza.

Olise, ambaye ana mkataba wa miaka mitano na Bayern, alifunga mabao 10 katika mechi 19 za Luigi Kuu England msimu uliopita, licha ya kukosa muda mwingi wa kucheza kutokana na majeraha.

"Michael Olise ni mchezaji ambaye anaweza kuleta mabadiliko na kuvutia watu wengi kupendezwa na aina yake ya uchezaji," alisema Mjumbe wa Bodi ya Michezo wa Bayern, Max Eberl, katika taarifa yake.

"Tunataka msukumo mpya katika timu yetu, nguvu mpya, mawazo mapya - hivyo ndivyo wachezaji kama Michael Olise wanavyosimamia. Wakati wa mazungumzo, haraka aliashiria kwamba anataka sana kujiunga na FC Bayern. Tunamsubiri kwa hamu sana. Ataboresha mchezo wetu."

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba winga huyo mwenye umri wa miaka 22, alikuwa akiwaniwa pia na Manchester United, Chelsea na Newcastle United, lakini hatimaye aliamua kuhama Bundesliga, akiunganisha safu ya ushambuliaji na namba tisa wa Bayern, Harry Kane.

"Hii ni changamoto kubwa na kile nilichokuwa nikitafuta," alisema Olise.

Mwenyekiti wa Palace, Steve Parish alisema katika taarifa yake: "Tunajivunia sana kile ambacho Michael amefanikisha akiwa Crystal Palace, klabu ambayo ameimarika sana kama mchezaji.

"Tunaheshimu nia yake ya kujijaribu zaidi katika kiwango cha juu zaidi cha soka duniani, na ningependa binafsi kumtakia kila la kheri kwa safari yake ijayo na Bayern Munich nchini Ujerumani ambayo nina uhakika sote tutaifuatilia kwa karibu."



## Yanga kuifuata Kaizer Chiefs

INATOKA UK. 24

Taarifa iliyotolea na klabu hiyo inaeleza kuwa timu hiyo imealikwa kwenye michuano maalum ya Toyota Cup, ambapo itacheza dhidi ya wenyeji wao, Kaizer Chiefs kwenye Uwanja wa Bloemfontein, Julai 28, mwaka huu.

Ikumbukwe kuwa Yanga iliialika timu hiyo katika mechi ya Kilele cha Siku ya Mwananchi, Julai 22, mwaka jana na kushinda bao 1-0, lililofungwa na Kennedy Musonda.

Rais wa klabu hiyo, Hersi Said, amesema ni fahari kwao kualikwa kwenye mashindano hayo na kuahidi kwenda kutoa upinzani.

"Tumefurahi sana kupata mwaliko huu wa kushiriki michuano ya Toyota Cup 2024. Mechi hii inaendeleza uhusiano kati ya timu zetu mbili kubwa barani Afrika, ambayo ilianza mwaka jana tulipowaalika Kaizer Chiefs kushiriki maonyesho yetu, kwenye mechi ya kirafiki iitwayo Wiki ya Mwananchi.

"Tumefurahishwa na mwaliko huu na tunaahidi kutoa mechi ya ushindani ambayo itatusaidia kujiandaa na msimu mpya wa 2024/25," alisema Hersi.

## Mo afunguka mazito usajili

INATOKA UK. 24

Singida Black Stars.

Kusajiliwa kwa mchezaji huyo kunafanya Simba iwe na wachezaji 12 wapya iliyowasajili kuelekea msimu ujao, saba wakiwa wageni na watano wazawa.

Wachezaji saba wa kigeni ni Jushua Mutale kutoka Power Dynamos ya Zambia, Steven Mukwala akitokea Asante Kotoko ya Ghana, Jean Charles Ahoa kutoka, Stella Adjame ya Ivory Coast, Debora Fernandes Mavambo kutoka Mutondo Stars ya Zambia, Augustine Okajepha, kutoka Rivers United ya Nigeria na Karaboue Chamou, akitokea Klabu ya Racing Club d'Abidjan ya Ivory Coast.

Wachezaji wazawa waliotangazwa mpaka sasa ni Lameck Lawi kutoka Coastal Union, Abdulrazack Hamza wa Super Sports ya Afrika Kusini, Valentino Mashaka, akitokea Geita Gold, Omari Omari aliyekuwa akikipiga na Mashujaa FC na Kagoma.

Msafara wa watu 30 wakiwamo wachezaji, benchi la ufundi na wafanyakazi wengine walitarajiwa kuondoa jana nchini saa 11:00 jioni kuelekea Ismailia, Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Klabu hiyo imesema kuwa kipa wake namba moja, Ayoub Lakred, ndiye mchezaji pekee ambaye hajajiunga nao kwenye msafara kwani anatarajiwa kujiunga nao kambini akitokea nchini kwao, Morocco.

# DODOMA JIJI FC YAMNASA GOLIKIPA WA KAGERA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji iko mbioni kumsajili kipa wa Kagera Sugar raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Alain Ngeleka, ambaye alionyesha uwezo mkubwa msimu uliopita wa Ligi Kuu.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa kipa huyo aliomba kuondoka na kuvunja mkataba licha ya kwamba ulikuwa unamalizika 2025.

"Hakuna shabiki yeyote wa kweli wa soka ambaye hajamuona kipa huyu. Ni kipa mzuri sana kutoka DR Congo, kusema kweli atatusaidia sana, na huu ni ushauri wa kocha wetu Mecky Mexime kwa sababu ameshaifundisha Kagera Sugar," alisema mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo, ambaye amebainisha watawatangaza rasmi hivi karibuni.

**Klabu hiyo pia imewaongeza mikataba wachezaji wake 10, ambao imeona wanaweza tena kuisaidia timu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano.**

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo, imeeleza wachezaji hao watаunganika na wale ambao itawasijili kwa ajili ya kuunda kikosi imara msimu ujao.

Wachezaji ambao wataendelea kusalia kwa 'Walima Zabibu' hao ni Yassin Mgaza, Fadhili Mwinyimvua, Emmanuel Martin, Zidane Sereli, Augustino Nsata, Anderson Kimweri, Robison Kamura, Ntenje Albano, Apollo Onyango, na Mwana Kibuta.

## MWAKA WETU!...



Kiungo wa Uruguay, Federico Valverde (kushoto), akiucheza mpira kuondoa hatari dhidi ya Kiungo wa Brazil, Joao Gomes, kwenye mechi ya robo fainali ya michuano ya Copa America iliyopigwa Uwanja wa Allegiant, Nevada nchini Marekani juzi na kumalizika kwa sare tasa. Uruguay ilifuzu hatua ya nusu fainali baada ya kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-2. **PICHA: MTANDAO**

## *Ufunguzi CDF Cup 2024 kwa Mkapa*

**Na Shufaa Lyimo**

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kwa wingi kushuhudia mashindano ya Kombe la Mkuu wa Majeshi (CDF Cup 2024), yatakayoanza Julai 20-30, mwaka huu kwenye viwanja mbalimbali, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano hayo, Brigedia Jenerali Said Hamis (pichani), alisema ufunguzi utafanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alisema lengo la mashindano hayo yenye kaulimbiu 'Ushindi ni Heshima', ni kuimarisha afya, umoja na mshikamano wa majeshi.

Alitaja michezo itakayochezwa kuwa ni mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, pete, ngumi pamoja na kulenga shabaha na kwamba yatashirikisha timu mbalimbali za majeshi ikiwamo kamandi ya anga, nchi kavu na ile ya Jeshi la Kujenga Taifa, JKT.

"Maandalizi yanaendelea vema kuelekea kwenye mashindano hayo naamini kutakuwa na upinzani mkubwa," alisema.



# Michezo

Jumanne Julai 9, 2024

Nipashe




Araujo aongeza pigo Barca UKURASA 22

**WE NATAKA MABAO!...**



Mwekezaji, rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji (kulia), akiteta jambo kwa msisitizo na mshambuliaji wa klabu hiyo, Freddy Michael 'Fungafunga', jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA**

## Mo afunguka mazito usajili wa kutisha Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Klabu ya Simba ikikamilisha usajili wa wachezaji wapya kwa kumtangaza kiungo mkabaji kutoka Singida Black Stars, Yusuph Kagoma huku mlinda lango wao raia wa Morocco, Ayoub Lakred, akisaini mkataba mpya wa mwaka mmoja, Mwekezaji, rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed 'Mo' Dewji, amesema ameamua kufanya usajili wa nguvu ili kurejesha heshima ya klabu hiyo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mo alisema amefanya usajili huo mkubwa kwa kuwashirikisha wataalam zaidi ya 50 kutoka nchi mbalimbali duniani, ikiwamo Tanzania.

"Naamini tumefanya usajili mkubwa na mzuri, haikuwa kazi rahisi, nimejaribu kuwasiliana na watu zaidi ya 50 kwa ajili ya usajili huu, nilishirikiana na maskauti kutoka nchi za Uholanzi, Ufaransa, na wengine hapa Tanzania kuweza kusajili wachezaji hawa.

"Kama mnavyoona timu safari hii ina vijana wengi sana, wanaanzia miaka 20 hadi 24 hivi, kwa hiyo nina imani kubwa tukienda kwenye maandalizi yetu, kikosi kikawa na muunganiko mzuri, watatuletea matokeo mazuri na kurudisha furaha yetu," alisema mwekazaji huyo.

Mo, alisema amefurahi kukutana na kuwaona wachezaji ambao amewasajili na wengineo, kwani wengi wao ni mara ya kwanza kukutana nao 'laivu'.

"Nimefurahi kwani, wachezaji wengi wametoka nchi mbalimbali, ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kukutana nao, pia nimepata bahati ya kukutana na kocha mkuu, benchi la ufundi, tulikuwa na mazungumzo mazuri, timu sasa inaanza kwenda Misri ya kwa ajili ya 'pre season', tutakaa pale siku kama 20 hivi, Mungu akitujalia tutarudi mwisho wa mwezi huu kwa ajili ya Simba Day, Agosti 3," alisema Mo.

Jana mchana, klabu hiyo ilimtangaza kiungo mkabaji, Kagoma, akisajiliwa kwa mkataba wa miaka mitatu kutokea, Singida Big Stars.

Kabla ya hapo, aliwahi kuichezea Klabu ya Geita Gold kisha kujiunga na Singida Fountain Gate, ambapo baadaye alikwenda Ihefu FC, ambayo imebadilishwa jina na kuitwa

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga kuifuata Kaizer Chiefs

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Yaalikwa kucheza Kombe la Toyota huku ikitangaza kumsajili kipa wa...

HATIMAYE, Klabu ya Yanga imetangaza kumsajili golikipa Abubakar Khomeiny, baada ya tetesi za muda mrefu, huku wakati wowote ikitarajiwa kwenda nchini Afrika Kusini kushiriki michuano ya Kombe la Toyota.

**Khomeiny, aliyesajiliwa kutoka Singida Black Stars, anatarajiwa kwenda kuchukua nafasi ya Metacha Mnata, ambaye taarifa zinaeleza kuwa hatokuwa sehemu ya kikosi msimu ujao baada ya mkataba wake kumalizika.**

Klabu hiyo imemtambulisha kipa huyo Mtanzania, baada ya awali kutangaza kumsajili beki wa kushoto raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Chadrack Boka kutoka FC Saint Eloi Lupopo ya nchini humo.

Beki huyo anatajwa kuja kuchukua nafasi ya Mkongomani mwenzake, Joyce Lomalisa, ambaye hatoendelea kuwapo tena kwenye kikosi hicho.

Khomeiny, anakuwa mchezaji wa nne kusajiliwa na Yanga kuelekea msimu ujao wa mashindano, akiwa ndiye Mtanzania pekee mpaka sasa.

Wengine waliosajiliwa na kutambulishwa rasmi ukimuacha Boka, ni Mzambia Clatous Chama na Prince Dube raia wa Zimbabwe.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema msimu huu hawatafanya usajili wa wachezaji wengi bali wachache, lakini ni maarufu na wenye uzoefu mkubwa katika michuano ya kimataifa.

"Tunasajili wachezaji wakubwa, maarufu kwenye maeneo ambayo tuna mapungufu, nilisema hatutasajili kwa mihemko, na tumethibitisha hilo, bado kuna wachezaji wapya ambao wataingia kwenye kikosi cha Yanga kuelekea msimu ujao," alisema.

Hata hivyo, taarifa zinasema kuwa mchezaji ambaye Yanga wanaweza kumtambulisha ni Jean Baleke aliyekuwa akiichezea Simba kabla ya kutimkia Al Ittihad Tripoli ya Libya.

Wachezaji wote wa Yanga walitarajiwa kuripoti jana kwa ajili ya kuanza kambi, kabla ya kutangaziwa utaratibu mwingine.

"Kuhusu maandalizi ya msimu na kambi, wachezaji wetu wataanza kuingia Jumatatu (jana), 'pre season' tutaweka wapi? Pale pale Kigamboni, au tutasafiri? Tutakuja kuwajuza," alisema.

Wakati hayo yakiendelea klabu hiyo imealikwa nchini Afrika Kusini kwa ajili ya michuano ya Toyota Cup.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >